

# KUCHAGUA BIBI-ARUSI



Wagonjwa wengi sana. Siwezi kuwafikia wote kwa wakati mmoja. Bali, sikilizeni.

<sup>2</sup> Hakika nina furaha kuwa hapa tena, usiku wa leo, katika jumba hili zuri la mikutano, miongoni mwa kikundi hiki cha watu wa ajabu. Nasi tulikuwa tukiingia, huko nje, dakika chache zilizopita, wale watu waliokuwa wamesimama nje barabarani walisema hawangeweza kuingia ndani. Nami nikasema, “Vema, huenda nikaweza kuwatafutia nafasi.” Nao hawangewaacha waje humu. Kwa hivyo nasikitika hatuna nafasi ya kutosha kwa ajili yao. Walisema orofa ya chini ilikuwa imejaa, pia. Na kwa hivyo tunasikitika kwa hayo. Bali tuna furaha kuwa hapa, na kufurahia kuona kikundi hiki chema cha wahudumu, wafanyi biashara hapa, nanyi nyote wajumbe kutoka mahali mbalimbali nchini.

<sup>3</sup> Nilikuwa na majaliwa makuu kuzungumza asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa, jambo ambalo nathamini kuwa ni heshima kuzungumza mbele ya watu wema kama hao. Nilizungumzia somo la: *Kapi Halitarithi Pamoja Na Ngano*. Sikuweza kulimaliza. Na halikuwa kosa la yu—yule ndugu. Yeye alijaribu kuwashawishi wasimamizi kuturuhusu kukaa muda mwingine zaidi, bali hakuweza kufanya hivyo. Hakika nathamini hilo, Ndugu Demos. Hilo ni zuri, zuri sana. Hakika nawashukuru kwa wema wenu, kila mmoja. Bali hawangeturuhusu tufanye hivyo. Kwa hivyo ilitulazimu tu ku—ilitulazimu kufunga. Nitachukua hilo, wakati mwingine, kumaliza huo: *Kapi Halitarithi Pamoja Na Ngano*. Je, mliuelewa huo, ninyi mliokuwa hapa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Natumaini kulikuwako ya kutosha kuufanya ueleweke.

<sup>4</sup> Sasa, najua, usiku wa leo, kuna mjadala, pia, kwa hivyo sitaki kuwaweka hapa muda mrefu hata muukose huo. Kwa sababu, nafikiri huo hakika ulikuwa muhimu sana kwa—kwa waaminio Wapentekoste, ule mjadala tuliouona hivi majuzi usiku. Kundi zuri sana la watu, majibu mazuri sana, wazi. Ilinifanya kujisikia vizuri sana, kuuona huo. Ninatumaini Bwana ataubariki, usiku wa leo. Na yeyote autazamaye, na waamini. Hayo yangekuwa ndiyo maombi yangu manyofu.

<sup>5</sup> Na ripoti nyingi sana zimekuja, leo, kutoka katika barua na simu, za watu wengi wanaoponywa katika mkutano huu. Nalifurahia hayo sana. Hiyo, hiyo ni, kuona wagonjwa, kwa namna fulani ndiyo huduma yangu.

<sup>6</sup> Na—naja hapa juu kuhubiri. Mimi, mnajua, mimi si mhubiri. Bali mimi, nikiwa na hii, sarufi yangu ya Kentucky, “ake, aiko” na—na maneno hayo yote, kwa hivyo si—siwezi kusema kama

mtu aitwaye mhubiri wa kisasa wa siku hizi. Ni—nisingeweza kupachukua mahali hapo, kwa sababu si—sina elimu.

<sup>7</sup> Bali mimi hupenda kuelezea yale niyuayo kuhusu Hilo, kwa wengine, ama yale najisikia nayajua kulihusu, kwa wengine, vile nimejifunza Hilo, jinsi Yeye alivyo kwangu. Yeye ndiye maisha yangu yote, yote ambayo ningetarajia kuwa, na mengine mengi zaidi kuliko vile nilivyowahi kuwaza, kwamba ingekuwa vigumu kupata rafiki, kamwe, duniani, nilipokuwa mvulana mdogo. Bali hakika nashukuru kwa ajili ya marafiki wakuu leo.

<sup>8</sup> Mimi ni . . . [Ndugu mmoja anasema, “Kuna shida kidogo kusikia huko nyuma, Ndugu Branham. Songea karibu.”—Mh.] Loo, samahani. Ki—kidogo niko kando hapa, mahali fulani, alisema.

<sup>9</sup> Sasa, kuingilia ibada moja kwa moja, hebu tufungue kwa ajili ya kusoma Maandiko fulani. Daima na—napenda kusoma Biblia, kwa sababu ni Neno la Mungu. Ninaamini hilo. Na ninaamini Hilo ni Neno la Mungu lisilokosea. Na sasa nina Maandiko machache yaliyoandikwa hapa chini, na muhtasari ambao ningetaka kurejea, kwa dakika chache, labda kwa dakika arobaini na tano.

<sup>10</sup> Ndipo basi tutaondoka kwa wakati mzuri kwenda kuona mjadala huu wa ajabu tena usiku wa leo. Na ninaamini ya kwamba Mungu ataendelea kuwabariki hata mwisho. Na ninajua mnayopaswa kufanya. Nami ninahitajiwa kwenda Tucson kwa motokaa, baadaye, usiku wa leo, mwaona, kwa hivyo mwaweza kuwazia. Hiyo ni safari ya saa kumi kwa motokaa.

<sup>11</sup> Na ninaondoka kwenda ng’ambo, na yanipasa kudungwa sindano ya homa ya manjano kwa majaribio asubuhi kwa serikali. Kwa hivyo ya—yanipasa kufika kule. Ilinibidi kuiahirisha, hivi majuzi, nao hawatakubali “la” kama jibu tena sasa. Pia nimebakiza kudungwa moja ya pepo punda pamoja na moja ya homa ya chawa, na ya kuniongeza nguvu.

<sup>12</sup> Kwa hivyo, nashukuru sana kwa fursa hii, na—na huu mkutano mzuri tuliokuwa nao kabla ya mikutano hii. Hakika ulisisimua moyo wangu. Ninyi ni kikundi chema cha watu. Natumaini ya kwamba Mungu atawabariki.

<sup>13</sup> Wakati saa iliyo kuu zaidi . . . Yule mnyama mkubwa mno anayekaa kule juu, aliyejibingirisha ghafla kule Alaska, siku chache zilizopita, alirusha mkia wake tena asubuhi ya leo, karibu na, huko chini karibu na Washington. Anaweza kuelekea huku, kwa urahisi sana. Na kama Roho Mtakatifu ataniambia dhahiri . . .

<sup>14</sup> Mtu fulani amekuwa akijibu . . . akiniuliza kwamba, “Je, itatendeka hapa, Ndugu Branham?” La, sijui hayo. Sijui kamwe, mpaka ninapojua. Hiyo ndiyo kweli.

<sup>15</sup> Kila mara ninataka kuwa mwaminifu kwenu. Mimi sitadhania, kuchukua mawazo yoyote, ama mengine, ninayoamini, ama kitu kama hicho. Nikiwaambieni, itatendeka. Vema, inampasa Yeye kuniambia, kwanza, ndipo nitawaambieni. Na—najua ulimwengu mzima uko katika hali ya kutikisika. Tuko katika wakati wa mwisho. Lakini kitu kimoja ambacho nimejaribu kuwa . . .

<sup>16</sup> Ndugu Shakarian alikuwa akisema asuhubi ya leo, jinsi alikuwa akipitia kwenye mistari ya maombi, na kufikia chini kule na kuchukua zile kadi kabla watu hawajafika, na kuzitazama, na kuona kama—kama niliwaambia yale waliyokuwa wameandika mle. Wao huandika vitu vya kila namna kwenye kadi zao za maombi, mwajua, naye alitaka tu kuona kama ilikuwa kweli. Alisema, toka kwa mamia aliyokuwa amechunguza, hapajakuwepo kosa hata moja. [Ndugu Shakarian anasema, “Hapajakuwepo na kosa hata moja.”—Mh.] Hapatakuwa na kosa hata moja, waona, kwa sababu, mradi—mradi tu ni Mungu. Kama nitajiingiza mwenyewe ndani yake, basi ni kosa papo hapo kwanza.

<sup>17</sup> Msichana mdogo ambaye baba yake ameketi, akinisikiliza sasa, alinjia, si muda mrefu uliopita. Alikuwa na ndoto. Akasema, “Ndugu Branham, ndoto hii maana yake nini?”

<sup>18</sup> Nikasema, “Sijui, dada. Itanibidi kutafuta kujua, kama Bwana ataniambia.” Basi nikaenda na kujaribu kumuuliza Bwana, Naye hakuniambia kamwe.

<sup>19</sup> Huyu msichana mdogo akarudi tena. Akasema, “Vema, sasa iko wapi tafsiri ya ndoto yangu?”

<sup>20</sup> Nikasema, “Njoo hapa, mpenzi, uketi chini.” Nikasema, “Baba yako na mama yako ni marafiki zangu wazuri sana. Unaona? Nao wamekuja kutoka mbali sana huko Canada, wamestaafu, na kukaa huku pamoja nami. Wanaamini haya, ninayotaribu kusema. Nami sijawahi kusema jambo lolote lisilo kweli kwa yeyote, makusudi, maishani mwangu. Kama ni . . . nafikiri najua maana ya hiyo ndoto. Lakini hadi nitakapona hiyo ndoto mimi mwenyewe, na halafu Yeye aniambie maana yake, siwezi kukwambia. Waona, nikijitungia tu jambo fulani, huenda kukawa na wakati ambapo utanihitaji kati ya uhai na kifo, na ndipo hungalijua kama utaniamini au hutaniamini.”

<sup>21</sup> Kama nikiwaambieni chochote katika Jina la Bwana, ni hivyo kweli. Huyu Ndiye aliyeniambia hayo. Na mpaka sasa, miaka hii yote, kote ulimwenguni, na ulimwenguni mwote, haijakosea hata mara moja. Sababu . . . Na, sasa, mwajua binadamu hawezi kuwa asiyekosea hivyo. Inahitaji Roho wa Mungu kufanya hayo.

<sup>22</sup> Na sasa nina Ujumbe ambao ninawajibikia. Na mara nyingi nimedhaniwa, miongoni mwa watu, vema, labda mtu fulani ambaye hakuketi chini na kuwazia tu kwa dakika moja, ya

kwamba mimi nilikuwa ni—ni, loo, mtu mbaya sana, ya kwamba sikuwapenda watu, na eti kila mara nawaudhi. Na hivyo sivyo. Hivyo sivyo. Nawapenda watu. Lakini, mwajua, upendo husahihisha.

<sup>23</sup> Kama mvulana wako mdogo alikuwa ameketi barabarani pale, nawe ukasema, “Kipenzi, mwanangu, sikutaki nje kule, lakini . . .” Na huku motokaa zikipita kasi karibu naye, nawe ukamuingiza ndani. Akakimbia nje tena. Mbona, yakupasa kumrudi. Iwapo unampenda, utafanya hivyo. Inakubidi.

<sup>24</sup> Kama ukiona mtu akielea mtoni, kuelekea maporomoko ya maji, katika mtumbwi mdogo, na unajua ya kwamba mtumbwi huo utazama ufikiapo kwenye maporomoko, je, ungelisema, “Yohana, wewe, labda yakupasa kuwaza kidogo, labda hutafaulu”? Kama ninajua hatafaulu, mimi karibu nitamvuta ghafla toka mtumbwini, ikiwa ninaweza, kwa sababu ni upendo unaotenda hayo.

<sup>25</sup> Na sasa, katika Jumbe hizi ninazonena, sijaribu kuingiza fundisho lolote, ama mengineyo. Mimi—mimi hufanya hayo katika kanisa langu mwenyewe. Bali huku nje miongoni mwa wanaume na wanawake ambao ni wa madhehebu tofauti na mawazo tofauti, mimi hujaribu tu kuileta kwa urahisi, kuelezea; lakini ya kutosha kufikia ambapo kama umezaliwa na Roho wa Mungu, ninaamini utaelewa ninayomaanisha, miongoni mwa Wakristo, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, na wengineo.

<sup>26</sup> Sasa, usiku wa leo, nataka kufungua Mwanzo, sura ya 24. Nataka kusoma . . .nikianza na kifungu cha 12 cha Mwanzo sura ya 24.

*Naye akasema, Ee BWANA, Mungu . . .bwana wangu Ibrahimu, nakuomba mambo yangu uyajalie yawe heri leo, ukamfadhili bwana wangu Ibrahimu.*

*Tazama! nimesimama hapa karibu na kisima cha maji, na binti za watu mjini wanatoka kuteka maji.*

*Basi na iwe hivi; yule msichana nitakayemwambia, Tua mtungi wako, nakuomba, ninywe; naye akasema, Unywe, nami nitawanyweshwa na ngamia zako pia; basi huyu na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako Isaka; na kwa hayo nitajua umenipa fadhili . . .kwa bwana wangu.*

<sup>27</sup> Halafu katika Kitabu cha Ufunuo. Huo ni mwanzo wa Biblia, Mwanzo. Sasa, katika mwisho wa Biblia, nataka kusoma katika sura ya 21 ya Ufunuo, na kifungu cha 9.

<sup>28</sup> Tunajua yale Maandiko haya ya Mwanzo hapa . . . Soma sura yote, ukitaka. Ni Mungu akimtuma Eliezeri. Ama, Ibrahimu akimtuma Eliezeri, samahani, kumchagulia Isaka bibi-arusi. Naye Rebeka mrembo akaja, na katika jibu kamilifu la maombi

ambayo—ambayo Eliezeri, mtumishi wa Ibrahimu, alikuwa tu ameomba.

Sasa katika kifungu cha 9 cha sura ya 21 ya Ufunuo.

*Akaja mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa saba vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena nami, akisema, Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana Kondoo.*

<sup>29</sup> Sasa ninataka kuchukua kwa ajili ya somo, usiku wa leo, kwa ajili ya hilo: *Kuchagua Bibi-Arusi*. Na hii ni, kama ndugu yangu ambaye hurekodi hapa akipenda, hii ni kanda ambayo unaweza tu kuisambaza.

<sup>30</sup> Na sasa, katika hii, haimaanishi kwamba mimi ninasema hili kwa kusanyiko hili lililopo hapa, bali kanda hizi huzunguka kote ulimwenguni. Zinatafsiriwa katika, karibu, loo, lugha nyingi sana, hata katika nchi za makafiri ulimwenguni kote. Sisi huzituma kanda hizi, bure, kama chama cha kanisa. Nazo zinatafsiriwa. Na kotekote kupitia misitu ya Afrika, na India, na hizi kanda husambazwa, ulimwenguni kote.

Sasa, kuchagua Bibi-arusi!

<sup>31</sup> Katika mambo mengi ya maishani sisi tumepewa chaguo. Njia ya maisha, yenyewe, ni chaguo. Tuna haki kufanya njia yetu wenyewe, kuchagua njia yetu wenyewe tunayotaka kuishi.

<sup>32</sup> Elimu ni chaguo. Tunaweza kujichagulia iwapo tutaelimishwa, ama iwapo hatutaelimishwa. Hilo ni chaguo tulilo nalo.

<sup>33</sup> Mema na mabaya ni chaguo. Kila mwanamume, kila mwanamke, mvulana na msichana, inampasa kuchagua iwapo watajaribu kuishi vyema ama hawataishi vyema. Ni chaguo.

Chaguo ni jambo kuu.

<sup>34</sup> Kikomo chako cha Milele ni chaguo. Na huenda ikawa, usiku wa leo, baadhi yenu watafanya chaguo hi—hilo, la mahali ambapo mtaishi Milele, kabla ibada hii haijaisha usiku wa leo. Kutakuwapo wakati mmoja, ambapo, kama ulimkataa Mungu mara nyingi, kutakuwapo wakati mmoja utakapomkataa mara ya mwisho. Kuna mstari kati ya rehema na hukumu. Na ni jambo la hatari kwa mwanamume ama mwanamke, mvulana au msichana, kuvuka huo mstari, kwa kuwa hakuna kurudi unapovuka mstari huo wa mwisho. Kwa hivyo, usiku wa leo, huenda ikawa ndio wakati ambao wengi watafanya uamuzi wa—wao, mahali watakapoishi Milele isiyo na mwisho.

<sup>35</sup> Kuna chaguo lingine tulilo nalo maishani, hilo ni, mwenzio wa maisha. Kijana mwanamume au kijana mwanamke, anayeingilia maisha, ame—amepewa haki ya kuchagua. Kijana mwanamume huchagua. Kijana mwanamke ana haki ya kukubali ama kukataa. Lakini lingali ni chaguo, pande zote

mbili. Wote wawili mwanamume na mwanamke, wana haki ya kujichagulia.

Pia, una chaguo, kama Mkristo.

<sup>36</sup> Una chaguo la kanisa, hapa Marekani, mpaka sasa, ambalo waweza kuhudhuria. Hiyo ni haki yako mwenyewe ya Kimarekani, kujichagulia kanisa lolote unalotaka kuwa mshirika wake. Hilo ni chaguo. Si lazima uhudhurie lolote la hayo, kama hutaki. Bali ukitaka kubadilisha kutoka Methodisti kuingia Baptisti, ama Katoliki kuingia Protestanti, ama chochote kile, hakuna mtu anayeweza kukwambia ama kukufanya uhudhurie kanisa lolote lile. Huo ndio ninii—huo ndio uhuru wetu. Hiyo ndiyo iliyo demokrasia yetu. Kila mtu anaweza kujichagulia mwenyewe. Uhuru wa dini, na hilo ni ja—jambo kuu. Mungu atusaidie kuuhifadhi muda mrefu tuwezavyo.

<sup>37</sup> Una chaguo pia. Kama... Unapochagua kanisa hili, unaweza kuchagua kama wewe, katika kanisa hili, kama utachagua kanisa ambalo litakuongoza hata kikomo chako cha Milele. Unaweza kuchagua kanisa ambalo lina kanuni fulani za imani, hata ukafikiri kwamba kanuni hizo ndizo kile unachotaka hasa. Ama, kanisa lingine lililo na kanuni zao za imani.

<sup>38</sup> Na ndipo kuna Neno la Mungu, una chaguo kwake. Inakupasa kuchagua.

Kuna sheria isiyoandikwa miongoni mwetu, ya kuchagua.

<sup>39</sup> Naamini ilikuwa Eliya, wakati mmoja, juu ya Mlima Karmeli, baada ya lile shindano la kuamua, katika saa kuu ya hatari sana ambayo tunakaribia sasa hivi. Labda, huenda ikawa kwako ama kwangu, usiku wa leo, kwamba tufanye chaguo hili, kama lile tukio la Mlima Karmeli. Kusema kweli, nafikiri linaendelea, ulimwenguni kote, sasa. Bali hivi punde kutakuwepo wakati ambapo itakulazimu kuchagua.

<sup>40</sup> Nanyi wanaume hapa, wa makanisa yenu ya kimadhehebu, aminini tu hili, ya kwamba ile saa imekaribia sana, ambapo itawabidi kuchagua. Ama mtaingia kwenye Baraza la Ulimwenguni, au hamtakuwa dhehebu tena. Itawalazimu kufanya hayo, na chaguo hilo linakuja hivi karibuni.

<sup>41</sup> Na ni jambo la hatari kungoja mpaka hiyo saa ya mwisho, pia, kwa sababu huenda ukajichukulia jambo ambalo hutaweza kujiondoa kwalo. Unajua, kuna wakati ambapo unaweza kuonywa, ndipo, ukivuka huo mstari wa onyo, basi tayari umetiwa alama upande huo mwingine, kupigwa chapa.

<sup>42</sup> Kumbuka, mwaka wa yubile ulipofika, basi ku—kuhani aliondoka akipiga baragumu yake, ya kwamba kila mtumwa angeweza kuwa huru. Bali kama walikataa kupokea uhuru wao, basi ilimpasa kupelekwa hekaluni, penye kizingiti, na kutobolewa sikio kwa uma, ndiposa akamtumikia bwana wake

siku zote. Iltiwa kwenye sikio lake kama mfano, wa kusikia. “Imani chanzo chake ni kusikia.” Yeye alisikia ile baragumu, bali hakutaka kuisikiza.

<sup>43</sup> Na mara nyingi, wanaume na wanawake husikia Kweli ya Mungu, na kuiona imethibitishwa na kuhakikishwa, kuwa Kweli, bali hata hivyo hawataki kuisikia. Kuna sababu nyingine. Kuna chaguo jingine walilo nalo, kuliko kukabiliana na Kweli pamoja na kanuni za mambo, kwa hivyo masikio yao yanaweza kuzibwa yasisikie Injili. Hawataisikia tena kamwe. Ushauri wangu kwenu, Mungu anapouzungumzia moyo wako, wewe kubali papo hapo.

<sup>44</sup> Eliya aliwapa chaguo, ambalo liliwakabili: “Chagueni hivi leo mtakayemtumikia. Mungu akiwa Ndiye Mungu, mtumikieni. Bali ikiwa Baali ni Mungu, mtumikieni.”

<sup>45</sup> Sasa, kama tunavyoona ya kwamba mambo yote ya kawaida ni mfano wa mambo ya kiroho, kama tulivyopitia katika somo letu asubuhi ya leo, kama jua na tabia zake. Hayo yalikuwa ndiyo Biblia yangu ya kwanza. Kabla sijasoma hata ukurasa mmoja kwenye Biblia, nilimjua Mungu. Kwa sababu, Biblia imeandikwa kila mahali katika maumbile, na yanalingana tu na Neno la Mungu: vile ambavyo kifo, kuzikwa, kufufuka kwa maumbile haya; na jua kuchomoza, kupita, kutua, kufa, kufufuka tena. Kuna mambo mengi sana ambayo tungefananisha, Mungu katika maumbile, ambayo hatuna budi kuyaruka, kwa ajili ya Ujumbe huu.

<sup>46</sup> Sasa, kama ya kiroho, ama, ya kawaida ni mfano wa ya kiroho, basi, kuchagua bibi-arusi, kwa maumbile, ni mfano wa kuchagua Bibi-arusi, yule Bibi-arusi, kwa kiroho.

<sup>47</sup> Sasa, ni jambo zito sana tunapoenda kuchagua mke, mwanamume, kwa kuwa nadhiri hapa ni “hata kifo kitakapotutenganisha.” Hivyo ndivyo inavyotupasa kuidumisha. Nawe unaweka nadhiri hiyo mbele za Mungu, kwamba ni mauti tu yatakawotenganisha. Nami nafikiri inatupasa... Mtu mwenye akili timamu, anayepanga maisha yake ya usoni, inampasa kuchagua mke huyo kwa uangalifu sana. Jihadhari unayofanya. Naye mwanamke anayemchagua mume, ama anayekubali chaguo la mume, inampasa kuwa mwangalifu sana kwa yale anayofanya, na zaidi sana siku hizi. Mwanamume yampasa kufikiria na kuomba kabla hajamchagua mke.

<sup>48</sup> Nafikiri, siku hizi, zilizo na visa vingi sana vya talaka sasa, kwamba tunaongoza ulimwenguni huku Marekani, katika visa vya talaka. Tunaongoza ulimwengu wote. Kuna talaka nyingi sana hapa kuliko kwingine kwote, taifa hili, na linasemekana, na kudhaniwa, kuwa taifa la Kikristo. Ni fedheha jinsi gani, mahakama zetu za talaka! Nafikiri, sababu yake, ni kwamba wanaume wamemwacha Mungu, na wanawake wamemwacha Mungu.

49 Na tunaona, ya kwamba, kama mwanamume aliomba na mwanamke akaomba juu ya jambo hilo; sio tu kuangalia macho marembo, ama mabega makubwa yenye nguvu, ama vitu kama hivyo, ama vivuto vingine vya ulimwengu; bali wangemtazama Mungu kwanza, na kusema, “Mungu, je, huu ni mpango Wako?”

50 Nafikiri, siku hizi, kuna udanganyifu mwingi sana, kama tu ilivyo shuleni. Watoto wanapo—wanapokuja, asubuhi, watoto wengi walio jirani, walio—walio marafiki zangu, watakuja na kusema, “Ndugu Branham, je, utatuombea? Tuna m—mtihani leo. Ni—nimesoma usiku kucha, na sioni kama—kama nimetosheka. Niombe.” Nafikiri ya kwamba mwanafunzi yeyote wa shule, kama ungeweza, kama. . . Na wazazi mezani asubuhi, ungeweza kusema, “Mama, Yohana ana mtihani leo. Hebu tumwombe sasa.” Ninafikiri hiyo ingeshinda yale yote ungeliveza kufanya kwa njia nyingine yoyote, ama kuchungulia karatasi ya mtu mwingine na kudanganyia, nafikiri, kama ungekuja tu na kuombea jambo hilo.

51 Na laiti tungechunguza yale tunayotenda wakati tunapoenda kuoana, tunapojichagua wake zetu, waume zetu, laiti tungeyachunguza kwa makini! Mwanamume yampasa kuomba kwa bidii sana, kwa maana anaweza kuangamiza maisha yake yote. Kumbuka, nadhiri ni “hata kifo kitakapotutenganisha,” naye angeweza kuangamiza maisha yake kwa kuchagua vibaya. Bali kama anajua ni nini, anachagua vibaya na anaoa mwanamke ambaye hastahili kuwa mke wake, naye anafanya hivyo haidhuru, basi ni kosa lake. Mwanamke akimchukua mwanamume naye anajua ya kwamba hafai kuwa mume wako, basi hilo ni kosa lako mwenyewe, baada ya kujua yaliyo mema na mabaya. Kwa hivyo, hupaswi kufanya hivyo mpaka utakapomba kwa bidii kabisa.

52 Ni jambo lile lile katika kuchagua kanisa. Sasa, huna budi kuomba juu ya kanisa unamoshiriki. Kumbuka, makanisa huwa na roho.

53 Sasa, sitaki kukosoa. Bali natambua kuwa mimi ni mzee, na sina budi kuondoka hapa, mojawapo ya siku hizi. Nami sina budi kuwajibika kwenye Siku ya Hukumu kwa yale ninayosema usiku wa leo ama wakati wowote mwingine. Nami, kwa hivyo, sina budi kuwa mkweli kabisa na kushawishika kabisa.

54 Bali, hebu nenda kanisani, na kama utachunguza tabia ya hilo kanisa, hebu mwangalie tu mchungaji kwa muda mfupi, na mara nyingi utaona ya kwamba kanisa hutenda kama mchungaji wake. Wakati mwingine, mimi hushangaa iwapo hatupati roho ya sisi kwa sisi badala ya Roho Mtakatifu. Unafikia mahali ambapo mchungaji ni mtu wa mapinduzi kwelikweli na mwenye vituko, utaona ya kwamba kusanyiko liko vile vile. Nitakuleta katika kanisa ambamo nimeona mchungaji akisimama, anatikisa kichwa chake huku na huko.



Hebu liangalie kusanyiko, wao hufanya vile vile. Hebu mchukue mchungaji, anayemeza kila kitu kwa pupa, kwa kawaida kanisa hufanya jambo lile lile. Kwa hivyo, kama nilikuwa ninachagua kanisa, ningalichagua kanisa la kweli, lenye mafundisho ya kimsingi, linaloamini Injili Yote, kanisa la Biblia, kama ningelikuwa nachagua moja kuwaingiza familia yangu. Chagua. Niliwaangalia . . .

<sup>55</sup> Wavulana, hivi majuzi, mwana wa Ndugu Shakarian pamoja na mkwewe, walinipandisha hapa kuombea jamaa mdogo, mwimbaji, mtoto wa watu. Alikuwa tu amerudi. . . Fred Barker, hilo ndilo jina lake, alikuwa tu amerudi kutoka safarini. Nao wakanipigia simu, ya kwamba, “Fred alikuwa yuafa.” Ndiposa, kabla sijaifikia ile nyumba, ujumbe mwingine ukaja, “Huenda amekufa sasa hivi.” Naye akasema alikuwa na ku—kutokwa na damu kwenye ubongo, naye alikuwa amepooza, na—na alikuwa yuafa, na mkewe alitaka mimi nimwombe.

<sup>56</sup> Nami nikawaza, “Loo, nikijaribu kuruka kwa ndege, yeye atakuwa amekufa kabla sijafika kule, na huenda amekufa sasa.” Kwa hivyo, nikapiga simu haraka na kumpata maskini yule mama kwenye simu. Na—na tukaiweka ile simu, kwenye sikio la Fred. Hangaliweza kumeza. Walimfanyia kumeza kwa mpira. Na tulipomwombea, alisema, akaashiria, ukatolewe kooni mwake. Angeweza kumeza. Madaktari hawakuamini hilo. Wakautoa, naye angeweza kumeza. Alikuwa ameketi, hivi majuzi.

Kanisa; kuchagua kanisa.

<sup>57</sup> Simu iliingia tu, muda mfupi uliopita. Asubuhi ya leo, mshiriki wa kanisa langu, ambaye hasa ni mwanamke Mbaptisti kutoka Louisville, alifariki mapema asubuhi ya leo. Na kanisa langu nyumbani, kikundi halisi cha watu waliowekwa wakfu, walikutanika pamoja na kuenda huko chini, kabla mwenye kutayarisha mazishi hajamtia dawa asioze, wakasimama mbele zake, wakaomba hata uhai ukamrudia. Naye yuaishi, usiku wa leo. Wazee wa kanisa langu, mbona, wamefundishwa kuamini ya kwamba mambo yote yanawezekana, wanamjia Mungu kwa uaminifu.

Kwa hivyo, lazima ufanye chaguo sahihi.

<sup>58</sup> Pia, aina ya mwanamke ambaye mwanamume atamchagua, itaonyesha malengo yake na tabia yake. Kama mwanamume akichagua mwanamke asiyefaa, inaonyesha tabia yake. Na kile anachojifunganisha nacho, kinaonyesha kilicho ndani yake kweli. Mwanamke huonyesha kilicho ndani ya mwanamume anapomchagua kuwa mkewe. Inaonyesha kilicho ndani yake. Haijalishi anayosema kule nje, tazama alichooa.

<sup>59</sup> Ninaenda kwenye ofisi ya mtu, naye anasema yeye ni Mkristo; picha zimebandikwa kotekote ukutani, ule muziki wa rumba ukiendelea. Sijali anayosema. Siamini ushuhuda wake, kwa sababu roho yake inalishwa kwa hayo mambo ya

ulimwengu. Vipi, tuseme, kama angelimwoa msichana mwimbaji wa bendi, ama vipi kama angalioa kipusa wa watu, ama mrembo tu, mhuni mamboleo? Inaonyesha. Inaonyesha yaliyo niani mwake, jinsi nyumba yake ya usoni itakavyokuwa, kwa sababu amemchukua kusudi akawalee watoto wake kwake. Na chochote alichu mwanamke huyo, hivyo ndivyo atakavyowalea watoto hao. Kwa hivyo, inaonyesha yaliyo ndani ya mwanamume huyo. Mwanamume anayemchukua mwanamke kama huyo, huonyesha tu anayowaza kuhusu maisha ya usoni.

<sup>60</sup> Je, waweza kumwazia Mkristo akitenda jambo kama hilo? La, bwana. Nisingewaza. Mkristo wa kweli hatawatafuta vipusa kama hao, na wasichana waimbaji wa bendi, na vidoshu wa watu. Yeye atatafuta tabia ya Kikristo.

<sup>61</sup> Sasa, huwezi kuwa na vitu vyote. Yawezekana kuweko na msichana mmoja ambaye ni mrembo sana. Na yule msichana mwingine, labda yeye ni. . . umbo lake linaonekana bora kuliko huyo. Basi huenda ikakulazimu kujinyima mmoja kwa ajili ya huyo mwingine, lakini, kama hana tabia ya mama, ya mwanamke. Na, yeye. . . Sijali kama yeye ni mrembo ama si mrembo. Ni heri uangalie tabia yake, awe mrembo asiwe mrembo.

<sup>62</sup> Sasa, kwa kuwa, inafaa, kama Mkristo angechagua mke, inampasa kuchagua mwanamke halisi, aliyezaliwa mara ya pili, haijalishi anavyoonekana. Ni kile alichu, ndicho kinamfanya. Na ndipo, pia, hiyo inaonyesha tabia yake mwenyewe ya kiungu, na inaonyesha kilicho niani mwake na yatakayotukia siku za usoni, kwani familia yake itakuzwa na mwanamke kama huyo, kwa ajili ya mipango yake ya usoni ya nyumba yake.

<sup>63</sup> Kama akioa mmoja wa hawa vipusa wahuni mamboleo, vidoshu wa watu, angetarajia nini? Ni nyumba ya namna gani mwanamume angetarajia kuwa nayo? Kama akioa msichana ambaye hana uadilifu kutosha kukaa nyumbani na kutunza nyumba, na anataka kufanya kazi huko nje katika ofisi ya mtu fulani, huyo atakuwa mtunza nyumba wa aina gani? Utakuwa na mayaya na kila kitu kingine. Ni kweli.

<sup>64</sup> Sasa, mimi sipendi sana hii tabia ya kisasa, ya wanawake kufanya kazi. Nilipoona hawa wanawake wenye hizi nguo rasmi, juu ya pikipiki, wakiendesha humu mjini, kama polisi, ni aibu kwa mji wowote utakaowaachilia wanawake kufanya hivyo. Mnaona? Mnaona? Huku wanaume wengi wakiwa hawana kazi, inaonyesha mawazo ya kisasa ya mji wetu. Inaonyesha kushuka kwa uadilifu. Haitupasi kuwa na wanawake hao huko nje namna hiyo. Hawana shughuli zozote huko nje namna hiyo.

<sup>65</sup> Mungu alipompa mwanamume mke, alimpa kitu kizuri kuliko vyote ambavyo angaliweza kumpa, nje ya wokovu. Bali mmoja aendapo kujaribu kuchukua mahali pa mwanamume,

basi yeye ni karibu kitu kibaya kuliko vyote ambavyo angaliweza kuvipata. Sasa, hiyo ni kweli. Mnaona?

Sasa tunaweza kuona matumizi ya kiroho.

66 Na—najua hiyo ni mbaya, unafikiri ni mbaya, bali ni Kweli. Hatujali ni mbaya jinsi gani, inatubidi kukabiliana na mambo yalivyo. Hivyo ndivyo Biblia inavyofundisha. Unaona?

67 Sasa, sisi hapa tunaona wazi wazi mpango wa kiroho, wa mpangilio wa Mungu kwa ajili ya Makao Yake ya usoni pamoja na Bibi—arusi Wake wa usoni, ukionekana sasa.

68 Kama mwanamume akimwoa kidosho wa watu, unaona kile anachotazamia siku zijazo. Mwanamume akimwoa mwanamke ambaye hatakaa nyumbani, unaona yale anayotazamia siku za usoni. Na mimi wakati mmoja. . .

69 Hili linasikika kuwa baya sana. Najisikia tu niliseme. Na mimi—mimi, kwa kawaida, ninapojisikia niseme jambo, yanipasa niliseme. Na kwa kawaida huwa ni njia ya Mungu.

70 Ni—nilizoea kwenda na mfugaji ambaye nilifanya kazi naye, kununua ng’ombe. Basi nikaona yule mzee kila mara alitazama moja kwa moja usoni mwa mtamba wa ng’ombe kabla hajaenda kumnadia. Kisha akakipindua kichwa chake, na kumtazama huku na huko. Nikamfuata, nikamtazama. Naye akamtazama juu chini, kama alionekana mzuri, kwa umbo. Ndipo akageuka na kumtazama usoni, na wakati mwingine angetikisa kichwa chake na kuondoka.

Nikasema, “Jeff, nataka kukuuliza jambo fulani.”

Akasema, “Endelea, Bill.”

71 Nami nikasema “Mbona kila mara unamtazama ng’ombe huyo usoni?” Nikasema, “Anaonekana mzuri, ng’ombe mzito mzuri—mzuri.”

72 Kasema, “Nataka kukuambia, ewe mvulana, una mengi ya kujifunza.” Nami ni—nikafahamu hilo baada ya yeye kuniambia. Kasema, “Sijali alivyoumbika. Huenda akajaa nyama ndi, mpaka kwenye kwato. Lakini akiwa na hayo macho jeuri usoni mwake, kamwe usimnunue.”

Nikasema, “Kwa nini hivyo, Jeff?”

73 “Vema,” kasema, “jambo la kwanza ni kwamba,” kasema, “yeye hatatulia kamwe.” Kisha akasema, “Jambo la pili ni kwamba, hatakuwa mama kamwe kwa ndama wake.” Tena akasema, “Wanamweka zizini sasa, ndiyo sababu yeye ni mnono. Hebu mfungulie, akiwa na hayo macho jeuri, angetimua mbio hata afe.”

74 Nikasema, “Unajua, kidogo nimejifunza jambo fulani. Naamini hayo yanahusu wanawake, pia.” Kweli. Kweli.

75 Hayo macho jeuri, yanayong’ara, ya kihuni, afadhali usimkaribie, ewe mvulana, hivyo vitu vyote vyenye rangi ya

samawati juu ya macho yake. Nami sikuninii . . . Nisingevitaka hivyo. Sidhani hivyo vinafaa kwa Mkristo. Sijali vipi televisheni na magazeti yanavyosema ni virembo. Ndicho kitu cha kuchukiza kuliko vyote, cha kutisha mno nilichowahi kuona maishani mwangu.

<sup>76</sup> Nilipoviona hivyo kwa mara ya kwanza, hapa katika Hoteli ya Clifton, asubuhi moja, kwenye kiamshakinywa . . . Naliona baadhi ya wasichana wakija. Ndugu Arganbright alikuwa tu ndiyo ameingia, na mimi. Naye alikuwa ameenda kwenye orofa ya chini. Nami nikatazama, ndipo msichana huyo akaingia. Nikawaza, “Vema, si—si—si—sijui.” Sikuwa nimeiona hapo kabla. Ilikuwa aina fulani. Loo, ilionekana kama ameoza, mwajua, kaonekana mtu wa kuchekesha. Sisemi hayo ili kuchekesha. Na—nasema hayo. Mwajua, nimeona ukoma. Mimi ni mmishenari. Nimeona aina zote za vioja, mwajua, jinsi magonjwa yalivyo. Nami nilitaka kumwendea huyo msichana na kumwambia, “Mimi—mimi—mimi ni mhudumu. Na—nawaombea wagonjwa. Je, u—ungetaka nikuombe?” Nami sikuwa nimewahi kuona kitu kama hicho. Ndiposa, hapa kukaja wawili au watatu zaidi, wakaingia. Kwa namna fulani nikarudi nyuma basi na kungojea.

<sup>77</sup> Naye Ndugu Arganbright akaja, kwa hiyo nikasema, “Ndugu Arganbright?” Huenda yupo hapa. Nikasema, “Je, ana shida gani mwanamke yule?” Unaona?

Naye akasema, “Hiyo, hiyo ni rangi.”

<sup>78</sup> Nikasema, “Vema, jamani, jamani!” Mnaona? Nilifikiri inawapasa kumweka kwenye hospitali ya maradhi mabaya mahali fulani, mwajua, asije akaambukiza wanawake wengine wote.

<sup>79</sup> Lakini, unajua, inakupasa kupanga, kuchunguza, kuomba, unapochagua. Kwa kuwa, tunaona, kwa hili, Neno la ahadi. Yeye, bibi—arusi ambaye mwanamume atamchagua, ataonyesha tabia yake. Inaonyesha kilicho ndani yake.

<sup>80</sup> Sasa, waweza kuwazia mwanamume, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, akichukua kitu kama hicho kuwa mkewe? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Si—si—sioni hiyo, ndugu. Sasa, labda mimi ni mzee tu mwenye kinyongo. Bali, wajua, si—siwezi kuelewa hilo kamwe, waona, tazama, kwa kuwa itaonyesha yaliyomo ndani yake. Huyo atamsaidia kutengeneza makao yake ya siku za usoni.

<sup>81</sup> Sasa, basi, tunapogeukia sasa kwa muda mfupi, upande wa kiroho. Basi unapoona kanisa lililoko ulimwenguni, likitenda kama walimwengu, likitamani ya ulimwengu, likishiriki ya ulimwengu, likihesabia Amri za Mungu kana kwamba Yeye hakuziandika kamwe, ndipo u—unaweza tu kuwaza ya kwamba Kristo hatachukua Bibi—arusi kama huyo. Je, ungewazia kuchukuliwa kwa hili kanisa la kisasa leo hii kama Bibi—

arusi? Sio na Bwana wangu. Sininii. . . Ni vigumu kwangu kuona hilo. Hapana. Kumbuka, sasa, mume na mkewe ni mmoja. Je, ungalijiunganisha mwenyewe na mtu kama huyo? Kama ungalifanya hivyo, hakika kidogo ingalivunja imani yangu kwako.

<sup>82</sup> Halafu, basi, vipi kuhusu Mungu kujiunganisha na kitu kama hicho, kahaba kupindukia wa kidhehebu? Unafikiri angefanya hivyo, “Wenye mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu zake”? Yeye hangefanya hivyo kamwe. Hana budi kuwa na tabia Yake ndani yake. Kanisa halisi, la kweli, lililozaliwa mara ya pili halina budi kuwa na ta—tabia iliyokuwa ndani ya Kristo, kwa sababu mume na mke ni mmoja. Na ikiwa Yesu alitenda yale tu yaliyompendeza Mungu, akatii Neno Lake na kudhihirisha Neno Lake, Bibi-arusi Wake itamlazimu kuwa na tabia ile ile. Bibi-arusi hangeweza, kwa vyovyote vile, kuwa dhehebu. Kwa sababu, basi, haijalishi ni kiasi gani unataka kusema, “sivyo,” hilo linaongozwa na halmashauri mahali fulani, ambayo huliambia litende nini na lisitende nini, na, mara nyingi, huwa umbali wa maili milioni moja kutoka kwa Neno la kweli.

<sup>83</sup> Ni vibaya sana kwamba tuliondoka kwa yule Kiongozi halisi ambaye Mungu alituachia kuongoza Kanisa. Yeye kamwe hakutuma wazee wa mikoa. Kamwe hakutuma maaskofu, makadinali, makasisi, mapapa. Alimtuma Roho Mtakatifu kwa ajili ya Kanisa, kuliongoza Kanisa. “Atakapokuja huyo Roho Mtakatifu, atawaongoza awatie kwenye Kweli yote, awafunulie mambo haya, ambayo nimewaambia, awakumbushe, na mambo yajayo atawapasha habari zake.” Roho Mtakatifu alikuwa afanye hivyo. Sasa, kanisa la kisasa linamchukia Huyo. Hawamtaki, kwa hivyo lingewezaje kuwa Bibi-arusi wa Kristo? Watu wa siku hizi wanachagua dhehebu la kisasa. Inachofanya, inaonyesha tu kuelewa kwao kubaya kwa Neno.

<sup>84</sup> Sikusudii kuudhi, ila nataka iingie ndani vya kutosha hata utaichunguza.

<sup>85</sup> Nimewaoza waume na wake wengi, lakini kila mara hunikumbusha juu ya Kristo na Bibi-arusi Wake. Mojawepo ya ndoa nilizounganisha hapa, wakati fulani uliopita, li—lilikuwa jambo kuu sana maishani mwangu. Imekuwa miaka kadhaa iliyopita, nilipokuwa tu ni mhudumu kijana.

<sup>86</sup> Ndugu yangu alikuwa akifanya kazi kwa—kwa PWA. Sijui kama yeyote anakumbuka huo, bado, au la, yeyote aliye mzee kama mimi. Na huo ulikuwa m—mradi ambao serikali ilikuwa nao. Naye ndugu yangu alifanya kazi kule, maili thelathini hivi. Walikuwa wakichimba maziwa fulani, mradi wa uhifadhi.

<sup>87</sup> Na kulikuwa na mvulana mmoja aliyefanya kazi huko, pamoja naye, aliyetoka Indianapolis, kama, loo, karibu maili mia moja juu ya Jeffersonville ambako mimi—mimi ninaishi, ama nilikoishi. Na palikuwa na. . . Akamwambia ndugu yangu, siku

moja, akasema, “Doc,” akasema, “Ni—ninataka . . . nitaoa, kama tu ningalipata fedha za kutosha kulipa mhubiri.” Akasema, “Ni—nina fedha za kutosha kugharamia hati yangu, lakini,” kasema, “sina fedha za kutosha kumlipa mhubiri.”

<sup>88</sup> Doc akasema, “Vema, ndugu yangu ni mhubiri, na—na a—anaweza kukuoza.” Akasema, “Yeye halipishi watu kwa vitu kama hivyo.”

Akasema, “Je, utamuuliza kama atanioza?”

<sup>89</sup> Vema, usiku huo ndugu yangu akaniuliza. Nikasema, “Iwapo hajaoa kamwe hapo mbeleni, mmoja wao hao wawili, nao ni . . . kila kitu kiko sawa.”

Akasema, “Vema, naam, nitamuuliza.”

Nami nikasema, “Kama ndivyo ilivyo, mwambie, aje huku chini.”

<sup>90</sup> Kwa hiyo, Jumamosi ilipofika ndipo huyo mvulana akaja. Limekuwa ni jambo kuu kwangu, kila mara kukumbuka jambo hili. Ningeninii . . . Alasiri yenye mvua, na motokaa iliyochakaa ya Chevrolet, ambayo mataa yake yalishikiliwa kwa waya, ikaja moja kwa moja, hapo mbele. Muda mfupi tu baada ya kifo cha mke wangu, nami nilikuwa nikiishi kama kapera, vyumba viwili vidogo. Na—naye Doc alikuwa huko pamoja nami, tukiwangojea.

<sup>91</sup> Ndipo—ndipo mvulana mmoja akatoka kwenye motokaa ile, na hakika hakuonekana kama bwana arusi, kwangu mimi, ama kwa yeyote yule, nadhani. Naam. Ningeweza kununua jozi nzuri ya viatu, kwa dola moja na nusu. Naye alikuwa na jozi, iliyochakaa kabisa. Na suruali yake ilikuwa yenye kupwaya mno. Naye alivalia moja ya haya makoti ya ngozi ya fuko. Sidhani wengine wenu wazee mngeweza kukumbuka. Lilionekana kana kwamba lilikuwa limepitishwa kwenye mtambo wa kufua nguo bila kukamuliwa, na lilikuwa na milia, limefungwa—fungwa *hivi*, pembeni juu.

<sup>92</sup> Ndipo m—msichana mdogo akatokea upande mwingine, amevalia ninii, loo, baadhi ya hizi nguo ndogo zenye mirabamiraba.

<sup>93</sup> Sijui. Nilikosea kuita aina hiyo ya kitambaa, wakati mmoja. Ging’amu, naamini ndivyo kinavyoitwa. Na kwa hivyo ilikuwa . . . [Kusanyiko linacheka—Mh.] Nimeitaja vibaya tena. Na—nafanya hivyo kila mara. Nami nikasema . . .

<sup>94</sup> Akatoka kwenye motokaa ile, na wakaja kwenye vipandio. Ba—basi walipoingia ndani, maskini msichana yule, yeye . . . nadhani, yeye, karibu yote aliyokuwa nayo tu ni sketi. Wala hakuwa na viatu, hata, miguuni. Alikuwa amesafiri kwa miguu kutoka Indianapolis huku akiomba lifti, akishuka kuja. Alikuwa na maskini nywele zilizing’inia chini, mgongoni, katika

misuko mirefu, iliyoning'inia mgongoni mwake. Alionekana mchanga sana.

Nami nikamwambia, “Je, wewe umetoshia umri wa kuolewa?”

<sup>95</sup> Akasema, “Naam, bwana.” Kisha akasema, “Nina kibali changu kilichoandikwa na baba yangu pamoja na mama.” Akasema, “ilinibidi kukionyesha ma—mahakamani hapa, kusudi nipate hati yangu.”

<sup>96</sup> Nikasema, “Vema.” Nikasema, “Ningetaka kuzungumza nanyi kidogo kabla ya kuunganisha ndoa hii.” Wakaketi. Yule mvulana akazidi kutazama huku na huku chumbani; alihitaji kukatwa nywele vibaya sana. Naye akazidi kutazama huku na huku chumbani. Hakuwa akinisikiza mimi. Nikasema, “Mwanangu, nakutaka usikize yale ninayosema.”

Kasema, “Naam, bwana.”

Nami nikasema, “Je, unampenda msichana huyu?”

Akasema, “Naam, bwana. Nampenda.”

Nikasema, “Nawe wampenda?”

“Naam, bwana. Nampenda.”

<sup>97</sup> Nikasema, “Sasa, una mahali pa kumpeleka baada ya kumuoa?”

Kasema, “Naam, bwana.”

<sup>98</sup> Nikasema, “Vema. Sasa,” nikasema, “nataka kuwaulizeni jambo fulani. Nasikia, unafanya kazi huku juu kwa hii PWA.”

Naye akasema, “Naam, bwana.” Hiyo ni kama dola kumi na mbili kwa juma moja.

Nikasema, “Unafikiri unaweza kumpatia riziki?”

Akasema, “Nitafanya yote niwezayo.”

<sup>99</sup> Nami nikasema, “Vema, hiyo ni sawa.” Kisha nikasema, “Sasa, vipi kama akiondoka kwenye... Vipi kama akipoteza kazi hii, dada? Utafanya nini, utatoroka urudi nyumbani, kwa mama, baba?”

Yeye akasema, “La, bwana. Nitakaa pamoja naye.”

<sup>100</sup> Nami nikasema, “Vipi, bwana, kama una watoto watatu au wanne, na huna cha kuwalisha, na huna kazi yoyote. Utafanya nini, utamfukuza?”

<sup>101</sup> Kasema, “La, bwana. Nitajitahidi zaidi. Tutafaulu, kwa vyovyote vile”.

<sup>102</sup> Nikajihisi duni. Ndipo nikaona ya kwamba kweli alimpenda msichana huyu, nao walipendana. Nikawaoza.

<sup>103</sup> Kisha nikashangaa alikompeleka. Siku chache, nikamuuliza ndugu yangu, Doc, kuwa ni wapi. Akasema, “Shuka uende New Albany,” mji mdogo chini yetu.

<sup>104</sup> Na kule chini mtoni, ambako nilikuwa nimeweka mabati, nilikoenda kila siku ni—nilipokuwa mchunguzi wa nyaya za nguvu za umeme. Kwa hivyo wakati watu wengine wote, wanapoketi chini, na kufanya mizaha na mengineyo, ningeingia ndani ya gari na kukimbia mbio mtoni na kuomba wakati huo, humo ndani, na kusoma Biblia yangu, chini ya kipande kikubwa cha mabati ambapo kiwanda cha chuma kilikuwa. Kuna mabehewa makuu-kuu kule.

<sup>105</sup> Basi jamaa huyu alikuwa ameenda kule chini na kujitwalia moja ya haya mabehewa na kujitengenezea mlango kwake. Na alikuwa amechukua gazeti na misumari yenye kofia.

<sup>106</sup> Ni wangapi wanaojua msumari wenye kofia? Basi, hamna Wakentaki hapa. Ni, chukua tu kipande cha kadibodi, kitie kijikofia, msumari bapa. Na ndipo ukipigilie ndani ya . . . Huo ndio msumari wenye kofia.

<sup>107</sup> Kwa hivyo, walikuwa wameiweka kote. Naye alikuwa amepanda kule juu kwenye kiwanda cha chuma na kujiokotea vikorokoro, na kujitengenezea kipandio, cha kupandia. Pia akaokota masanduku yaliyochakaa, na kujitengenezea meza. Nami nikawaza, siku moja, “Nitashuka niende nikaone wanavyoendelea.”

<sup>108</sup> Yapata miezi sita hapo mbeleni, nilimwoza binti wa E. V. Knight kwa mwanawe E. T. Slider. E. V. Knight, mmoja wa watu matajiri sana walioko kwenye Mto Ohio, na, loo, husimamia viwanda vikuu kule, vya kutengenezea hizi nyumba za kuunganishwa, na kadhalika. Na—naye Slider, E. T. Slider, ana kampuni ya kokoto na changarawe, watoto wa mamilionea. Nami nilikuwa nimewaoza.

<sup>109</sup> Nami nikarudi mahali fulani, nikajizoeza hayo yapata muda wa majuma mawili, na kurudi kwenye kibanda na kupiga magoti kwenye mto. Na sherehe zote na mengineyo niliyopata kupitia, karibu, yalizonibidi kupitia, kusudi nikamwoze huyo mume na mke! Na walipojitokeza, mbona, walikuwa . . . Mume na mke huyu mwingine walisimama tu pale katika chumba kidogo kikuu-kuu ambapo tulikuwa na kitanda cha kupumzikia na kitanda kilichokunjwa, bali wote waliozwa kwa sherehe ile ile.

<sup>110</sup> Ndipo basi, siku moja, niliwaza ningeshuka niende nikawatembelee hawa mke na mume matajiri. Haikuwalazimu kufanya kazi, baba zao walikuwa mamilionea, walikuwa wamewajengea makao mazuri. Hakika, huyu E. V. Knight, juu, hapa kilimani, vinundu vya milango yake vina kipimo cha kumi na nne cha dhahabu kwenye jumba lake kuu, kwa hivyo waweza kuwazia aina ya makazi wanamoishi. Haikuwalazimu kufanya kazi. Walikuwa wakipewa motokaa nzuri aina ya Cadillac kila mwaka. Na hakika, ni watoto tu, na walikuwa na kila kitu walichotaka. Nilipotembelea huko siku moja . . .



111 Sasa, nilivyofahamiana nao, mmoja wa rafiki zao alikuwa rafiki yangu msiri. Ni kama sote tuliunganika pamoja. Na hivyo ndivyo nilivyopata kuwajua, waliponitaka niwaoze.

112 Kwa hiyo nikaenda kuwatembelea. Nikashuka kutoka kwenye Fordi yangu kuu-kuu, nje, na kupanda vipandio. Ndipo—ndipo nikafika, kidogo karibu kupita kiasi, nami nikawasikia. Nao walikuwa wakigombana vikali. Walioneana wivu. Walikuwa wametoka kwenye dansi. Yeye alikuwa msichana mrembo kwelikweli. Tena kwa namna fulani alikuwa mmoja wa hawa malkia wa urembo. Alishinda tuzo nyingi sana kule, na kupata motokaa kadhaa na kadhalika, kwa kuwa malkia wa urembo. Nami nikawatazama, na mmoja alikuwa ameketi kwenye kona moja na mwingine kona nyingine, wakigombana mvulana fulani ambaye alikuwa amecheza dansi naye, ama msichana fulani, kitu fulani.

113 Nilipoingia, wakaruka upesi sana na kushikana sakafuni, mi—mikono yao, sakafuni, wakatembea wakija mlangoni. Kasema, “Naam, u hali gani hapo, Ndugu Branham! Unaendeleaje?”

Nikasema, “Vyema. Mwaendeleaje nyote?”

114 Na “Loo,” mume akasema, “Mimi—mimi. . . Tuna furaha sana. Sivyo, mpenzi?”

Naye mke akasema, “Naam, mpenzi.” Unaona?

115 Sasa, unaona, unajivika jambo lisilo halisi. Sasa, huwezi kupata joto kwa moto uliochorwa, kama baadhi ya haya makanisa yanayojaribu kuchora pentekoste, ya jambo lililotendeka miaka elfu moja iliyopita ama miaka elfu mbili iliyopita. Huwezi kupata joto kwa moto uliochorwa. Pentekoste ni halisi tu leo kama ilivyokuwa wakati ule. Unaona? Naam. Ule Moto ungali unashuka. Si moto wa kuchorwa. Ni Moto halisi.

116 Kwa hivyo, hao, hao tu hapo. Unaona? Si—singelitaka kuishi hivyo.

117 “Loo,” nikawaza, “unajua, chini tu ya lile genge na kule kwenye mto, hapo ndipo wengine wawili walikoenda.” Naliwaza, “Jumamosi moja alasiri nitajipenyeza kule chini na kuona vile walivyokuwa wakiendelea.”

118 Kwa hiyo mimi, mchafu usoni, huku nimevalia surupwenye chafu, nimebeba vifaa vyangu. Nikawaza, “Nitawatembelea kisiri.” Nilijipenyeza kwa siri kana kwamba nilikuwa nikichunguza mipira ya kufunikia nyaya za nguvu za umeme zilizokatwa na radi ama kitu kingine, na huku nikitembea karibu na waya wa simu, nyaya za umeme mtoni. Na ile pale Chevrolet iliyochakaa, ilikuwa mbele ya nyumba. Yapata mwaka mmoja baadaye, baada ya kuwaoza. Na kulikuwa na—na. . . Mlango ulikuwa wazi, nami ningeweza kuwasikia

wakizungumza. Kwa hivyo hii yasikika kama mnafiki, bali nilisongea karibu vya kutosha hata niliweza kusikiza, kuona yale waliyokuwa wakisema. Nikasimama pale. Nami ninataka tu kujua, mimi mwenyewe.

<sup>119</sup> Ninapenda kuchunguza na kuwa na hakika kwamba nayafahamu yale ninayonena habari zake. Hivyo ndivyo nifanyavyo kuhusu Neno la Mungu. Ni Kweli, ama si Kweli? Je, Yeye atatimiza Neno Lake, ama hatimizi Neno Lake? Kama hatimizi Neno Lake, basi Yeye si Mungu. Unaona? Yeye hutimiza Neno Lake, Yeye ni Mungu. Unaona?

<sup>120</sup> Na kwa hivyo ninataka kuona vile walivyokuwa wakiendelea. Ndipo nikanyemelea kando-kando, pole pole sana. Nikamsikia yule mume akisema, “Loo, mpenzi, nilitaka kukununulia hiyo, sana.”

<sup>121</sup> Mke akasema, “Tazama, sasa, mpenzi.” Akasema, “Nguo hii yatosha.” Akasema, “Mbona, hii ni nzuri tu.” Kasema, “Nashukuru kwa hayo. Lakini unaona . . .”

<sup>122</sup> Nikajipenyeza karibu, ili niweze kuchungulia kwa mwanya, ambapo mlango ulikuwa umefunguliwa kule kwenye lile behewa. Naye huyo hapo, ameketi mle ndani, na mkewe pajani mwake; amemkumbatia, naye mke amemkumbatia. Naye alikuwa na moja ya hizi kofia za kale kama tarai, na alikuwa ametoboa kishimo kidogo, na akaibofya ndani, sehemu ya juu, naye akatoa mshahara wake, ndani humo. A—alikuwa ameziweka mezani. Akasema, “*Hizi* ni za vyakula. *Hizi* ni za bima. Na *hizi* ni za motokaa.” Nao hawangeweza kukimu mahitaji yao yote. Nikagundua, alikuwa ameona gauni dogo huko dukani, alikuwa amelitazama-tazama kwa majuma kadhaa, ambalo liligharimu dola moja na kitu. Alitaka kulinunua. Akasema, “Vema, mpenzi, ungeonekana mrembo sana kwa hilo.” Kisha akasema . . .

<sup>123</sup> Naye akasema, “Lakini, mpenzi, ni—nina gauni. Hakika si—silihitalaji.” Mnaona? Ndipo maskini malkia huyo . . .

<sup>124</sup> Nikarudi nyuma, na kutazama juu. Ningeweza kuona m—mnara juu ya ile nyumba nyingine. Nikasimama pale na kutazama, kwa dakika chache. Nikawaza, “Ni nani tajiri?” Nikawaza, “Kama, Bill Branham, ukitaka kuchukua mahali, ungeenda wapi?” Kwangu mimi, singechukua kile kitu cha kupendeza kule juu kilimani. Ningelichukua mtu huyu hapa chini, kama mjenzi halisi wa nyumba, mtu aliyenipenda na kukaa pamoja nami, mtu aliyejaribu kujenga nyumba; bila kukukamua kwa kila kitu, kwa ajili ya umaridadi; na mtu aliyekuwa pamoja nawe, aliye sehemu yako.

<sup>125</sup> Hiyo daima imedumu nami, ya jinsi hayo yalivyokuwa. Mmoja alimchagua msichana mrembo, huyo mwingine akachagua tabia nzuri. Sasa, hivyo tu ndivyo unavyoweza

kuchagua. Kwanza, tafuta tabia; na ndipo, kama unampenda, vema.

<sup>126</sup> Tazama, Adamu wa kwanza wa Mungu hakuwa na chaguo lolote, la mke wake. Hakupata chaguo. Mungu alimfanyia tu mmoja, naye hakupata kumchagua. Ndipo tunaona ya kwamba alimwongoza vibaya mbali na Neno la Mungu. Yeye hakupata kuombea jambo hilo. Ye—ye—yeye si kama wewe na mimi. Hakupata chaguo. Na pia, kwa kutenda hayo, akamwondoa kwenye mahali pake panapofaa kama mwana wa Mungu. Naye alitenda hayo kwa kumwonyesha njia ya kisasa zaidi ya maisha, jambo ambalo hakika hawakupaswa kufanya. Lakini tabia yake ilionyesha ya kwamba mke alikuwa amekosea. Malengo yake na shabaha zake zilikuwa mbaya hasa. Naye akamshawishi, kwa hoja zake, kwamba ile nuru mpya ya kisasa ambayo alikuwa amepata, ambayo ilikuwa kinyume na Neno la Mungu, ilikuwa njia bora zaidi ya kuishi.

<sup>127</sup> Na ni wanawake wangapi leo, na vile vile, wanaume, ambao wangeweza kumwondosha mwanamke mzuri kwa Mungu, ama kumwondosha mwanamume mzuri kwa Mungu? kwa kujaribu kumwambia, “Dini hii, enyi wavulana wa Kipentekoste, dini hiyo,” wao husema, “loo, hiyo ni ya mtindo wa kale, ni ukungu wa kale, usiamini hiyo.” Heri uombe kwa bidii kabla hujamwoa msichana huyo. Sijali yeye ana sura nzuri jinsi gani. Na mwanamume pia.

<sup>128</sup> Yeye alimshawishi kuacha mapenzi ya Mungu na kumfanya atende jambo ambalo haikumpasa kutenda, na, kwa hilo, akasababisha mauti kwa jamii yote ya binadamu. Hiyo ndiyo sababu Biblia inamkataza kufundisha, ama kuhubiri, ama kushughulikia Neno la Mungu, kwa njia yoyote.

<sup>129</sup> Najua, kina dada, wengi wenu husema, “Bwana aliniita kuhubiri.”

<sup>130</sup> Sitabishana na wewe. Bali nitakuambia, Neno linasema haikupasi kufanya hivyo. “Hatafundisha, ama kutwaa mamlaka yoyote, bali yampasa kuwa kimya.”

“Vema,” unasema, “Bwana aliniambia nifanye hivyo.”

<sup>131</sup> Silitilii hilo shaka hata kidogo. Je, mlisikia Ujumbe wangu hivi majuzi usiku kuhusu Balaamu? Balaamu alipata uamuzi wa kwanza, waziwazi wa Mungu, “Usitende hayo.” Bali aliendelea kujipumbaza hata mwishowe Mungu akamwambia aende akatende hayo.

<sup>132</sup> Mungu anaweza akakuruhusu kuhubiri. Sisemi hakufanya hivyo. Bali si kulingana na Neno Lake la asili pamoja na mpango. “Kwa sababu yampasa awe mtiifu, kama isemavyo torati.” Ni kweli. Kwa hivyo, hapaswi kufanya hivyo.

<sup>133</sup> Sasa, angalia tena jinsi bibi-arusi wa kawaida alivyo mfano wa wa kiroho. Neno linasema, ya kwamba, “Mwanamke

alifanyika kwa ajili ya mwanamume, wala si mwanamume kwa ajili ya mwanamke.”

<sup>134</sup> Sasa nitazungumza, na kwa nini, kwa dakika chache, juu ya Bibi-arusi wa Kristo, bali ninajaribu kuwaonyesha msingi wake.

<sup>135</sup> “Mwanamke alifanyika kwa ajili ya mwanamume, wala si mwanamume kwa ajili ya mwanamke.” Hiyo ndiyo sababu, chini ya torati ya kale, ambapo kuoja wanawake wengi kulikuwa halali. Mwangalie Daudi akiketi kule chini mwenye wake mia tano, na Biblia ilisema, “Alikuwa mtu aliyependeza moyo wa Mungu.” Akiwa na wake mia tano, naye Sulemani akiwa na elfu moja, bali hapana mmoja wa hao wanawake angaliweza kuwa na mume mwingine.

<sup>136</sup> Chukueni kanda yangu kuhusu *Ndoa na Talaka*. Ambapo, juu ya mlima kule Tucson, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa kule juu nikiomba kwa ajili yake. Wao waliruhusu wanafunzi waondoke shuleni, wakaitazame ile Nguzo ya Moto ikizunguka ule mlima na kufanya umbo la faneli, mbele nyuma, juu chini. Watu wa karibu hapa wanajua hayo, hapo, na wakaiona; Nayo ilinini. . . aliponiambia ukweli kuhusu haya maswali ya ndoa na talaka. Kama kuna upande mmoja unaoenda *hivi*, na mwingine unaoenda *vile*, hapana budi kuwepo na Kweli mahali fulani. Baada ya ile Mihuri Saba, Yeye alionyesha Ukweli wake ulivyo.

<sup>137</sup> Angalia, sasa, yeye asingeweza kuwa na zaidi ya mume mmoja, kwa sababu, “Mwanamke alifanyika kwa ajili ya mwanamume, wala si mwanamume kwa ajili ya mwanamke.” Wote hao wanawake mia tano walikuwa tu ni mke wa Daudi, nayo ilikuwa ni mfano. Kristo atakapoketi kwenye Kiti cha Enzi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, Bibi-arusi Wake hatakuwa mtu mmoja, bali itakuwa ni makumi ya maelfu, Bibi-arusi, wote katika Mmoja. Naye Daudi alikuwa na wake wengi, kama watu binafsi, bali wote pamoja tu walikuwa ndio mke wake. Kama vile Mwili wote wa waaminio ni Bibi-arusi wa Kristo, maana ni Yeye, mwanamke. Yeye alikuwa Mwanamume. Sasa, sisi tulifanyika kwa ajili ya Kristo. Kristo hakufanyika kwa ajili yetu.

<sup>138</sup> Hivyo ndivyo tunavyojaribu kufanya siku hizi katika vitabu vyetu vya kiada, ni kujaribu kufanya Neno (ambalo ni Kristo) litufae sisi, badala ya sisi kujaribu kujifanya wanaofaa kwa Neno. Hiyo ndiyo tofauti.

<sup>139</sup> Mtu anapomchagua msichana fulani kutoka kwa familia fulani, hapaswi kutegemea urembo, kwa kuwa uzuri wa uso hudanganya. Na urembo, urembo wa kisasa wa ulimwenguni, ni wa ibilisi.

“Loo,” namsikia mtu fulani akisema huko nje, “jihadhari hapa, mhubiri!”

<sup>140</sup> Nasema ya kwamba mambo haya katika ulimwengu huu, yanayoitwa marembo, ni ya ibilisi kabisa. Nitawathibitishieni. Basi, kwa minajili ya tamshi hili, hebu na tuchunguze Neno

takatifu la Mungu, kuona kama hilo ni kweli ama si kweli. Na baadhi yenu wanawake mnataka kuwa warembo sana! Angalieni unakotoka. Hapo mwanzo, tunaona ya kwamba Shetani alikuwa mrembo sana hata akawadanganya Malaika. Naye alikuwa Malaika mwenye sura nzuri sana kushinda wengine wote. Iliyonesha, inatokana na ibilisi. Methali ilisema, Sulemani alisema, “Uzuri unapita upesi.” Hiyo ni kweli. Dhambi ni maridadi. Hakika, ndivyo ilivyo. Inavutia.

<sup>141</sup> Nataka kuwaulizeni, na kuwaambieni jambo fulani hapa. Ninawatakeni mwone, kwa dakika chache. Katika spishi zote ulimwenguni, ndege, wanyama, tunaona ya kwamba katika maisha ya wanyama, wote isipokuwa wanadamu, ni wa kiume walio maridadi, na si wa kike. Mbona hivyo? Mwangalie nanii. . . Mwangalie kulungu, du—dume mkubwa wa kupendeza na pembe zake, na maskini jike lake kaidi. Mwangalie ku—kuku, kuku mdogo, mwenye madoadoa, na jimbi mzuri mwenye manyoya. Mwangalie ndege wa kiume na ndege wa kike. Mwangalie bata mwitu wa kiume na wa kike. Unaona? Na hamna spishi hata moja ulimwenguni, aliyumbwa, awezaye kudanganya na kujidunisha kama mwanamke.

<sup>142</sup> Sasa, dada, usiamke na kuondoka. Ngojewa tu mpaka tusikie mwisho wa Hili. Unaona? Unaona?

<sup>143</sup> Hapana chochote, hamna jike lolote mbali na mwanamke, linaloweza kuwa zinifu. Mnamuita mbwa “mzembe,” mnamwita nguruwe mwitu “ji—jike,” bali, kwa uadilifu, wana uadilifu mwingi kuliko nusu ya wachezaji mashuhuri wa sinema hapa nje. Hawawezi kuwa chochote kile ila waadilifu.

<sup>144</sup> Na mwanamke alikuwa ndiye aliyebadilishwa, kwa ajili ya upotovu. Hiyo ni kweli. Unaona mahali urembo unamwelekeza? Sasa, hiyo ndiyo sababu kwamba, siku hizi, tunaona kwamba urembo wa wanawake unaongezeka. Hebu mchukue Pearl Bryan, je, mliwahi kuona picha yake? Alidhaniwa kuwa mrembo mkuu wa Marekani. Hamna mtoto yeyote wa shule kutoka shule yoyote ambaye hangalimweka kwenye safu ya nyu—nyuma. Je, mnajua ya kwamba inapaswa kuwa hivyo? Je, mlujua ya kwamba Biblia inasema ya kwamba hivyo ndivyo itakavyokuwa?

<sup>145</sup> Je, mnajua ya kwamba kule kuanguka kulikuja kupitia kwa wanawake hapo mwanzo? Na kuanguka. . . Mwisho utamalizikia vile vile, wanawake wakiingia mamlakani na kuwatawala wanaume, na kadhalika. Mnajua Maandiko yanasema hivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnajua, siku atakapovalia nguo za mwanamume, na kukata nywele zake, mambo hayo yote ni kinyume na Neno la Mungu. Na je, mnajua yeye anawakilisha kanisa? [“Naam.”] Ukitazama yale wanayofanya wanawake, mtaona yale kanisa linayofanya. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, sasa, hiyo ni kweli tu kama Neno la Mungu lilivyo kweli.

<sup>146</sup> Hamna jike lingine ambalo limefanywa linaloweza kujishusha kama mwanamke anavyoweza kujishusha. Na hata hivyo, kupitia hapo, kwa ajili ya kufanywa kutoka . . .

<sup>147</sup> Yeye hakuwa katika ule uumbaji wa asili. Majike wengine wote walikuwa kwenye ule uumbaji wa asili: ndege, wa kiume na wa kike; wanyama, wa kiume na wa kike. Bali, katika maisha ya binadamu, Mungu aliumba mwanamume pekee, Naye akatoa kutoka kwake. Basi mwanamke ni kiumbe kilichotoka kwa mwanamume, kwa sababu Mungu hakuanzisha kitu kama hicho. Chunguza Maandiko. Ni kweli kabisa. Mungu, la, bwana, katika uumbaji Wake wa asili. Mwanamke aliwekwa nje kule.

<sup>148</sup> Lakini akiweza kusimama imara, ni thawabu kuu jinsi gani aliyo nayo kuliko mwanamume. Yeye amewekwa mahali pa majaribu. Kupitia yeye kikaja kifo. Yeye ana hatia kwa ajili ya vifo vyote. Lakini basi Mungu akageuka na kumtumia mmoja kurudisha Uzima tena; akamleta Mwanawe kupitia mwanamke, aliye mtiifu. Lakini aliye mbaya ni m—mwovu kuliko chochote kilichopo; hakuna kitu kinachoweza kuwa duni hivyo.

<sup>149</sup> Kaini, mwana wa Shetani, alidhani kwamba Mungu alikubali urembo. Anadhani hivyo siku hizi. Kaini alikuwa mwana wa Shetani. “Loo, sasa!” unasema. Hatutaingilia hilo kwa kina, bali hebu nikutatulie tu. Biblia ilisema yeye “alikuwa wa yule mwovu.” Kwa hivyo, hiyo yatosha. Vema. Sasa, yeye alikuwa mwana wa Shetani. Naye alidhani ya kwamba, kuingiza madhabahu na kuyafanya maridadi sana kwa kuabudia, hiyo ndiyo Mungu angeheshimu.

<sup>150</sup> Wao wanawaza, wanawaza jambo lile lile siku hizi. Hakika. Hili, “Tunajenga jengo kubwa. Tutakuwa na madhehebu makubwa. Tutajifanyia jengo lililo kubwa zaidi na watu waliovalia nadhifu kuliko wote, makasisi waliostaarabika kuliko wote.” Wakati mwingine Mungu yuko umbali wa maili milioni kumi kutoka kwake. Hiyo ni kweli. Ingawaje, ni kanisa.

<sup>151</sup> Kwa hivyo, ikiwa Mungu anaheshimu tu ibada, unyofu, sadaka, Kaini alikuwa mwenye haki tu kama Habili alivyokuwa. Bali ilikuwa ni kwa ufunuo, ambapo alielewa ya kwamba walichokula wazazi wake si matofaa.

<sup>152</sup> Nitasema jambo hapa ambalo halionekani zuri kwa mhudumu, bali nitalisema, haidhuru. Mimi huwasikia hawa wengine wakisema mambo, wakifanya mizaha midogo. Siikusudii. Nilisema haya, hata hivyo, “Kama kula matofaa kuliwafanya wanawake wajue walikuwa uchi, ni afadhali tusambaze matofaa tena.” Unaona? Uaona? A-ha. Samahani kwa hayo, bali kusudi tu libadilike. Nimewashikilia hapa, huku nikinena kuhusu wanawake, na kadhalika. Na—na—nataka kuwaburudisheni kwa dakika moja, kwa ajili ya yale yanayofuata. Sasa, tazama, wewe. . . Haikuwa matofaa. Tunajua hayo.

153 Kanisa limekuwa katika siku hizi, na mafanikio yake, kama mafanikio mengine yote yaliyobuniwa na mwanadamu, linakuwa la kisayansi. Wanajaribu kutengeneza kanisa la kisayansi, la kuvutia kwa picha pamoja na minara mikubwa. Na ni vibaya sana kwamba Wapentekoste waliingia katika mkondo huo. Mngelikuwa afadhali zaidi mkiwa na tari, kule pembeni, na Roho wa Mungu akiwazunguka. Lakini mnajaribu kujilinganisha na hao wengine, kwa sababu mmekuwa dhehebu. Hiyo ndiyo iliyosababisha hilo. Mnaona? Makanisa yanajaribu kuwa ya kisayansi.

154 Basi kumbuka, mwanadamu anavyopata usitawi kwa sayansi, ndivyo anavyojiua kila siku. Alipovumbua baruti, angalia kile ilichofanya. Alipovumbua motokaa, inaua zaidi ya vile baruti inavyoua. Sasa amejipatia kombora la haidrojeni. Unashangaa atakayofanya na hilo? Naam.

155 Ndivyo lilivyo kanisa, linavyojaribu kufanikiwa kwa sayansi, kwa mipango ya kujibunia ya binadamu, inakupeleka mbali zaidi kutoka kwa Mungu, na kukuingiza mautini, kuliko ilivyokuwa kwanza. Hiyo ni kweli. Usichague kanisa lako ulivyochagua mke wako. Unaona? Yale sayansi iliyomfanyia yalikuwa ajabu, bali ni afadhali ujiepushe na kanisa lako katika hayo; alitengeneza rangi, poda, na vitu hivi vingine vyote. Chagua kwa tabia ya Neno Lake.

156 Sasa hebu na tulinganishe bibi-arusi wa kawaida wa siku hizi na anayejiita bibi-arusi wa kanisa wa siku hizi. Linganisha mwanamke, anayeenda akaolewe siku hizi.

157 Sasa, angalia tu yale sayansi imemfanyia. Yeye hujitokeza, kwanza, akiwa amezikata nywele zake, na moja wa mitindo hii ya nywele ya Jacqueline Kennedy, unaona, ama kitu kama hicho. Na unajua Biblia inavyosema? Biblia hakika inampa mwanamume, akitaka, haki ya kumwacha kwa talaka, kama akifanya hivyo. “Ni mwanamke mwenye sifa mbaya, ambaye atazikata nywele zake.” Biblia ilisema hivyo. Kweli. Hamkujua hilo? En-he? Loo, naam! Ninahubiri sana California kwenu kutokujua hayo. Hiyo ni kweli. Loo, naam! Inanifaidi nini? Wanafanya hivyo, haidhuru. Huwezi kumchukua nguruwe na kubadilisha jina lake, kumfanya mwana-kondoo. Tazama.

158 Mtanichukia baada ya haya, bali mtaijua Kweli. Unaona?

159 Tazama. Hebu tuvilinganishe. Huyu hapa yuaja amejaa rangi, kitu ambacho siye, bibi-arusi wa kisasa. Mnawishe uso wake, mume angelimtoroka, labda. Angekushtusha mno, ukiondoa rangi hiyo yote kutoka kwake. Vivyo hivyo kanisa kubwa, lililopakwa rangi upande wa mbele, theolojia moto moto ya Wauza Vipodozi. A-ha. Wote wawili wana u—uso mrembo, bandia, urembo uliobuniwa na binadamu wala si urembo uliofanywa na Mungu. Hamna tabia ya kutosha kwa yeyote wao.

<sup>160</sup> Tazama, kama tu Shetani, ya kutosha kudanganyia, mlinganishe bibi-arusi wa kisasa naye sasa: anavaa kaptura, anajipaka rangi, anakata nywele zake, huvalia nguo zinazoonekana kama wanaume, na kumsikiza mchungaji aliyemwambia hayo ni sawa. Yeye ni mdanganyifu. Ataadhibiwa kwa hayo huko ng'ambo. Hiyo ni kweli. Anafanya hayo kudanganya, kujifanya kitu asicho.

<sup>161</sup> Hivyo ndivyo kanisa litendavyo, wanapata D.D., Ph.D., L.L.D. kubwa. Kwa hiyo mnasema, "Mchungaji wetu ni *hivi, vile na vinginevyo*," huenda hamjui Mungu zaidi ya Mhottentonti anavyojua hekaya za Kimisri. Hiyo ni kweli. Kweli. Ana baadhi ya ujuzi wa seminari ya theologia, bali hamjui Mungu hata kidogo.

<sup>162</sup> Kanisa la kisasa na rangi zao za kitheolojia, hmm, wana wanawake wao wote ambao utukufu wao umenyolewa, na akina riki wao na wachungaji walio nao, kama Yezebeli ikiwa kulikuweco mmoja. Nywele zilizokatwa, kaptura, rangi, vyote vimetengenezwa kwa ladha ya kitheolojia, hivyo ndivyo kanisa linavyosimama. Kweli. Bali tabia yake ya kiroho iko mbali sana na kule kuwa mtunzaji nyumba ambaye Yesu Kristo anakuja kumpokea.

<sup>163</sup> Kama Mkristo yeyote angemwoa mwanamke kama huyo, inaonyesha kuwa ameinguka kutoka kwa neema. Ladha yake ya Mungu na ladha yake ya makazi, jinsi makazi yanavyopaswa kuwa, iko mbali, anapomchagua mwanamke kama huyo. La, bwana. Hakika asingeridhisha ladha ya Mkristo. Tabia yake ya kiroho iko kwenye kiwango cha chini kabisa, amekufa, katika urembo wa kimadhehebu na tamaa ya ulimwengu.

<sup>164</sup> Hapo hasa ndipo kanisa linaposimama siku hizi, limemuuzia Shetani tabia yake liliyopewa na Neno, kwa ajili ya dini ya kisayansi ya kujibunia. Ambapo, lilikuwa na haki, kama kanisa la Mungu, kudumu na Neno la Mungu na kuwa na Roho Mtakatifu akitenda miongoni mwao, akiunganisha ule mwili pamoja na Neno na upendo wa Mungu. Badala yake, likauza haki yake ya mzaliwa wa kwanza, kama Esau, na kuchukua dhehebu, ambalo lingemruhusu kutenda hayo, chochote alichotaka, naam, kusudi tu lipate kupendwa na watu kama mama yake alivyofanya kule Nikea, Rumi. Neno la Mungu!

<sup>165</sup> Loo, jinsi imeingia katika milki yetu ya Kipentekoste! Ni vibaya sana, bali ilifanyika hivyo.

<sup>166</sup> Angalia, kwa muda mfupi, mtawa katika kanisa katoliki. Mwanamke huyo, ili kuwa mtawa, na anapochukua ule utaji wa mwisho, yeye amejitolea kabisa kwa kanisa hilo. Yeye (nafsi, mwili, na roho) ni mali ya kanisa hilo. Yeye hana nia yake mwenyewe. Hawezi kuwa nayo, anapochukua utaji huo wa mwisho, hana nia yake mwenyewe, hana hiari yake mwenyewe.



Tazama nje hapa, kwamba Shetani hufanya walio wake wa uongo, kama walio wa kweli.

167 Kanisa la kweli la Kristo, Bibi-arusi, amejitolea sana Kwake na kwa Neno Lake lililoahidiwa, hata nia ile ile iliyo ndani ya Kristo imo ndani yako. Ni tofauti jinsi gani!

168 Na tunaona leo hii, kwamba, kanisa la kisasa, kanisa la kisasa la ulimwengu, kanisa la kisasa la ulimwengu na pia kwamba lile Kanisa la kiroho yote mawili yametiwa mimba, kuzaa wana.

169 Mmoja wao, uzazi wa kidhehebu, utafanyika, moja ya siku... ili...siku hizi, katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, ambalo litauzalia ulimwengu yule mpinga Kristo, kupitia dhehebu. Hiyo ni Kweli kabisa. Huenda nisiishi kuona hilo. Naamini nitaliona. Bali, ninyi vijana, kumbukeni ya kwamba mlimsikia mhudumu akisema hivyo. Hiyo hatimaye itaishia. Na hiyo ni ile alama ya mnyama, atakapounda hilo Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Naye atamzaa mwanawe, yule mpinga Kristo.

170 Lile lingine limetiwa mimba kwa Neno la Mungu na litauzaa Mwili, ule Mwili uliokamilika wa Yesu Kristo, ambao ni Bibi-arusi. Mwili wa Kristo haujakamilika bado. Ni wangapi wanajua hilo? Mwanamume na mwanamke ni mmoja. Naye Kristo ni Mwili mmoja, Neno. Bibi-arusi itambidi kuwa sehemu iliyobakia ya Mwili huo. Na hao wawili, pamoja, wanafanya Mwili huo mmoja tena. Kama Adamu alivyokuwa hapo mwanzo: mwanamume, mkewe, ni mmoja. Sasa, Yeye, yule Bibi-arusi wa kweli, amejitolea Kwake sana, hata hatumii tena nia Yake mwenyewe. Nia Yake, hakika, ni mapenzi Yake, nayo mapenzi Yake ni Neno Lake.

171 Sasa mwangalie huyu anayedhaniwa kuwa bibi-arusi aliyechaguliwa na binadamu, na ulinganishe wa kiroho na wa kawaida wa siku hizi, Yezebeli wa kisasa aliyerogwa na Ahabu wake, urembo wa Wauza Vipodozi, na kila kitu. Liangalie kanisa, vile vile, lakini malaya kwa Neno la Mungu aishiye; madhehebu makubwa, majengo makubwa, fedha nyingi, mshahara mnono, wamejiuza kabisa. Watu wanasimama mimbarani wakiidhinisha kuwa hayo ni sawa, na kuwaacha waendeleo nayo. Udanganyifu mtupu, hivyo tu. Hakika ni Wakati wa Kanisa la Laodikia lililo kipofu, jinsi hasa Biblia ilisema lingekuwa. "Kasema, 'Mimi ni tajiri. Nimeketi kama malkia. Sina haja ya kitu.' Nawe hujui ya kuwa wewe ni maskini, mwenye mashaka, kipofu, mnyonge, uchi: nawe hujui." Kama hiyo si BWANA ASEMA HIVI, Ufunuo 3, sijaisoma kamwe. Hivyo ndivyo alivyo, wala hajui! Wazia hayo.

172 Kama ungelimwambia mwanamume ama mwanamke, barabarani, aliyekuwa uchi wa mnyama, na kuwaambia walikuwa uchi, nao wakasema, "Shika lako," mbona, pana

upungufu wa akili hapo mahali fulani. Ubongo wao una kasoro fulani.

<sup>173</sup> Na unapoweza kusoma Neno la Mungu, ambavyo inawapasa watu kufanya, na huu ubatizo wa Roho Mtakatifu tulio nao leo, na, watu, mbona, wanakutazama kana kwamba ulikuwa mwendawazimu. Unawaambia: “Mna...” Hawana budi kuzaliwa mara ya pili. Inawapasa kuamini Biblia.

<sup>174</sup> Wao wanasema, “Hiyo ilikuwa hekaya ya Kiyahudi, miaka mingi iliyopita. Kanisa letu linayo njia.” Wanyonge, wenye mashaka, vipofu, uchi, na hata hawajui. Ni... Na Biblia ilisema hiyo ndiyo hali wanayoifikia.

Nabii wa kweli angekosaje kuona hayo? Sijui.

<sup>175</sup> Inaingia moja kwa moja kwa makanisa yetu yote, kila mahali. Hebu iangalie tu, kwenye mwelekeo wa kisasa hasa. “Yule kahaba mzee na binti zake,” wa Ufunuo 17, akiwapa wale watu “maskini, vipofu, wenye mashaka” mafundisho yake ya theolojia kinyume na Neno la Mungu. “Nao wakakuta ndani yake nafsi za watunwa, na wanaume na wanawake wa—wa kila mahali.” Badala ya kuwavutia watu...

<sup>176</sup> Kristo huthibitisha Neno Lake, ambalo huvutia watu. Yeye hawavutii watu kwenye makanisa ambao huvutiwa na madhehebu makubwa na tamasha kuu, na mambo makuu yasiyofaa pamoja na vitu vya kuvutia macho. Bali Neno la Mungu humvutia Bibi-arusi wa Kristo.

<sup>177</sup> Sasa tazama. Inapendeza ku—kuona jinsi ambavyo—ambavyo kanisa linajaribu kuvutia macho ya watu kwa majoho mazuri na kwaya zenye mavazi rasmi, na wanawake waliokata nywele zao na nyuso zilizopakwa rangi. Nao wanadhani... Nao waliimba kama Malaika. Wakadanganya kama ibilisi, wakizurura-zurura usiku kucha kwenye dansi, bila kuwaza lolote kuhusu hayo. Na hayo ndiyo wanayowazia, “Ni sawa. Hayo ni mazuri.” Bali, unaona, hayo ni ya bandia. Hayo si Neno la Mungu.

<sup>178</sup> Huku, Bibi-arusi wa kweli huyavutia macho ya Mungu, kwa kutii Neno Lake. Tazama sasa. Sasa hebu tumwangelie Kristo.

<sup>179</sup> Unasema, “Vema, sasa, ngoja kidogo, vipi kuhusu uzuri huu unaonena habari zake?”

<sup>180</sup> Biblia ilisema, katika Isaya 53:2, ya kwamba, Yesu alipokuja, “Hakuwa na uzuri, hata tumtamani Yeye.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hana uzuri. Kama angalikuja katika uzuri wa kilimwengu, kama Shetani alivyo siku hizi, watu wangelimkimbilia na kumkubali jinsi wafanyavyo kanisa siku hizi. Wangalimwamini, na kumpokea, jinsi wanavyofanya Shetani siku hizi. Hakika, wangempokea. Bali Yeye hakuja katika uzuri wa aina hiyo, bali Yeye daima huja katika uzuri wa tabia. Hapo, Kristo hakuwa Mtu mzuri,

mkubwa, mwenye nguvu, mnene. Mungu hachagui watu wa aina hiyo.

<sup>181</sup> Nakumbuka wakati mmoja nabii aliondoka kwenda ku—kuchagua mfalme, kumfanya mwana wa Yese mfalme, akachukue mahali pa mfalme mwingine, Sauli. Ndipo basi Yese akamleta, mvulana wake mkubwa, mrefu, mzuri. Akasema, “Taji itaonekana sawa, kichwani mwake.”

<sup>182</sup> Nabii alienda kumtia mafuta. Akasema, “Mungu amemkataa.” Naye akamkataa kila mmoja wao, hata alipomfikia maskini mtu mdogo, mwenye mabega yaliyojikunyata, mtu mwekundu. Naye akamtia mafuta, na kusema, “Mungu alichagua huyu.” Unaona? Sisi huchagua kwa macho. Mungu huchagua kwa tabia.

<sup>183</sup> Tabia, hapajakuwepo na tabia kama ya Yesu Kristo. Inaishi ndani yako na kumdhihirisha Yeye. Tunaona hiyo ni kweli. Si uzuri Wake wa kilimwengu unaomvutia Bibi-arusi Wake. Ni tabia Yake, tabia ya Kanisa, ndiyo Yesu anatafuta; si penye majengo makubwa, penye madhehebu makubwa, penye washiriki wengi. Aliahidi kukutana nao popote wawili watatu wamekusanyika pamoja. Hakika. Hapo ndipo mwaminio wa kweli huweka matumaini yake, ni katika hilo Neno la Mungu linalodhihirishwa katika Kweli, ilivyo. Walichaguliwa kwa Neno Lake, si kundi linalopenda ulimwengu. Wanauchukia huo.

<sup>184</sup> Si ajabu hilo limetalikiwa Naye, kwa sababu limeukosa ufunuo Wake, na halina. Yeye halijali, jinsi linavyotenda na kufanya, na ni kiasi gani cha mambo haya ya kilimwengu lilicho nacho.

<sup>185</sup> Yeye anaangalia tabia yake, ile tabia ya Kristo. Sasa, hebu kidogo tu sasa. Ndivyo ilivyo. Yeye huchagua Bibi-arusi ili akaonyeshe tabia Yake, ambapo makanisa ya kisasa hakika hukosa mpango Wa—Wake hapa, maili milioni moja, maana wao wanakataa *Hili* kuwa Kweli. Kwa hivyo ingewezekanaje? Sasa, anatazamia siku ambayo huyo Bibi-arusi ataumbika, Waebrania 13:8, jinsi hasa ilivyokuwa, jinsi Yeye alivyokuwa. Haina budi kuwa mwili Wake ule ule, mifupa ile ile, Roho yule yule, kila kitu kile kile, kujengeka vile vile tu, na ndipo hao wawili basi wanakuwa kitu kimoja. Hata kanisa litakapokuwa hivyo, bado hawajakuwa mmoja. Tabia Yake, lile Neno, la wakati huu, halina budi kufinyangwa. Bibi-arusi hana budi afinyangwe kama alivyo Yeye.

<sup>186</sup> Sasa, katika kufunga, nataka kusema sababu ya mimi kusema mambo haya, ndipo nita—nitafunga. Hivi majuzi usiku, yapata saa tisa alfajiri, niliamshwa.

<sup>187</sup> Nataka yeyote wenu kujibu hili. Je, nimewahi kuwaambia chochote katika Jina la Bwana ila kilicho kweli? Imekuwa kweli daima. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi anisaidie, Mungu anajua hiyo ni kweli. Hapana chochote, popote

ulimwenguni, katika maelfu ya mambo ambayo yamesemwa, ambapo Yeye alikosea hata kwa neno moja. Daima imetendeka kikamilifu.

<sup>188</sup> Hata nilipokuwa Phoenix, hivi majuzi, ama ilikuwa yapata mwaka mmoja uliopita, na nikawaambia kuhusu ule Ujumbe juu ya—juu ya *Ni Wakati Gani, Mabwana?* Na nikawaambia, “Malaika saba wangekutana kule nje,” na ingekuwa ni kule kufunguliwa kwa hii Mihuri, na chochote kile. Na hapo ga—gazeti la *Life* likaandika makala juu yake, Mwali huu mkuu uliopaa hewani, maili thelathini kwenda juu, upana wa maili ishirini na saba. Wakasema hawakujuu ilikuwa nini; hawajui bado. Na watu wanaoketi papa hapa katika jengo hili usiku wa leo, walikuwa wamesimama pale pale pamoja nami ilipotendeka, vile hasa ilivyosema. Aliniambia kuhusu mambo yatakayotendeka, na yakatendeka vile hasa. Jinsi kila mmoja wa ile Mihuri ulivyofunuliwa, na kueleza habari za zile siri zilizofichwa kotekote kwenye zile nyakati za warekebishaji na kadhalika, kikamilifu kabisa.

<sup>189</sup> Jinsi ambavyo, wakiwa wamesimama juu ya kilima, watu, watatu au wanne wao wanaosimama mumu humu sasa, naam, wengi kuliko hao. Nilipokuwa nikipanda kilima kile, Roho Mtakatifu akasema, “Twaa jiwe lile.” Tulikuwa tukiwinda. Akasema, “Litupe juu hewani, na useme, ‘BWANA ASEMA HIVI.’” Nikafanya hivyo. Kutoka chini kule kukaja upepo mdogo wa kisulisuli. Nikasema, “Katika muda wa saa ishirini na nne, mtaona mkono wa Mungu.” Watu wanaoketi papa hapa sasa.

<sup>190</sup> Keshoye, yapata saa nne, tukiwa tumesimama pale, nikasema, “Iweni tayari. Ingieni kule chini ya motokaa,” mzee mwenye maarifa. Nikasema, “Jambo fulani linakaribia kutendeka.” Anga ilikuwa shwari, moja kwa moja katika genge kuu. Moto wa kisulisuli ukashuka toka Mbinguni, wenye sauti kuu sana, ukazipiga kuta namna hiyo. Ni—nilikuwa nimesimama moja kwa moja chini Yake. Nikatoa kofia yangu, nikashika kichwa changu. Ukaja yapata futi tatu au nne juu yangu, na kuchimba shimo kote kuzunguka ule ukuta hivyo, na ukalipuka. Ndipo ukarudi juu hewani, na kuzunguka—zunguka tena, na kushuka chini, mara tatu, hata ulikuwa umekata vichaka vya mesketi kule, umbali wa yadi mia mbili. Mnawasikia jamaa hao wakisema, “Amina”? Walikuwa kule ilipotendeka, mwaona, nao ukalipuka mara tatu.

<sup>191</sup> Walipotoka chini ya zile motokaa na kila kitu, wakarudi kule, walisema, “Kama hicho kingalikupiga, hungesalia hata doa.”

<sup>192</sup> Nikasema, “Ilikuwa—Ilikuwa ni Yeye. Alikuwa akinena nami.” Mungu hunena kwa upepo wa kisulisuli. Unaona? Na kulikuweco Nguzo ile ile ya Moto mnayoiona kwenye picha, imesimama pale.

Ndipo ilipopaa juu, wao wakasema, “Ni nini?”

Nikasema, “Hukumu inaipiga Pwani ya Magharibi.”

<sup>193</sup> Siku ya pili baadaye, Alaska nusura izame. Mnaona? Ukapiga mara moja, pale, pigo la kwanza.

<sup>194</sup> Ambapo, huna budi kufanya jambo fulani, kuiainisha. Kama yule mtu aliyetia chumvi kwenye chupa, na kuitupa majini, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, na kuwe na maji matamu.” Na mwingine, Yesu, alichukua maji na kuyamimina kwenye mtungi, na—na kutengeneza divai kwayo.

<sup>195</sup> Huna budi kuwa na kitu fulani, kuiainisha. Hicho ndicho hilo lilikuwa, lilitupwa juu hewani na kurudi chini. Hilo lilianzisha kile kisulisuli kidogo. Katika muda wa saa ishirini na nne, ulikuwa umetikisa huo mlima hata ukachimba mtaro kuuzunguka.

<sup>196</sup> Kasisi Bw. Blair anayeketi hapa, ninamwangalia moja kwa moja sasa, alikuwa kule juu na akachukua baadhi ya vipande vyake, na kadhalika. Hapa yupo Terry Sothmann, hao, na wanasimama hapa, na Billy Paul. Na ndugu, baadhi ya wengi wa hawa wengine wanaoketi hapa ndani, waliokuwa pale pale kuyaona yakitendeka ulipoupasua.

<sup>197</sup> Hiyo si hadithi. Hiyo ni kweli. Hiyo haikuwa kule nyuma katika siku za Biblia. Hiyo ni sasa. Mnaona? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu yeye yule ambaye daima amenionyesha mambo haya, nayo yametimia, kikamilifu kabisa. Hayajakosa kutimia hata mara moja. Sasa ninajivunia Yeye.

<sup>198</sup> Majuma machache yaliyopita, nilikuwa katika ono. Nami nilikuwa nimesimama mahali pa—pa juu, na ilikuwa nionyeshe kukaguliwa kimbele kwa Kanisa. Ndipo nikaona, likija kutoka ninii wangu... nilikuwa nimesimama *hivi*, nimeelekeza uso wangu Magharibi. Na wanawake wazuri sana walikuwa wakija upande *huu*, waliovalia vazi zuri kwelikweli, nywele ndefu zilizotengenezwa vizuri huku nyuma, nguo zenye mikono mirefu, na sketi ndefu nadhifu. Nao wote walikuwa wakipiga hatua taratibu, kama, “Twendeni, askari Wakristo, tukitembea kama waendao vitani, msalaba wa Yesu ukitangulia.” Na walipokuwa wakipita, nalisimama, na kulikuwa na Kitu pale, Roho fulani, alikuwa ni Mungu, ndipo akasema, “Huyo hapo Bibi-arusi.” Nami nikatazama, na moyo wangu ukafurahahi. Naye akazunguka *hivi*, na kupita nyuma yangu.

<sup>199</sup> Baada ya kitambo kidogo, huyo bibi-arusi aliporudi *huku*, ikasema, “Sasa kanisa la kisasa litakaguliwa kimbele.” Na hapa likaja kanisa la Asia. Sijapata kuona kundi chafu kama hilo.

<sup>200</sup> Haya hapa makanisa yale mengine yanakuja, ya mataifa mbalimbali. Walikuwa wa kuchukiza.

<sup>201</sup> Nami na—nasema haya kwa maana ninawajibika kusema kweli, mbele za Mungu. Naye aliposema, “Hili hapa kanisa la

Marekani linakuja sasa, likakaguliwe kimbele,” kama nimewahi kuona kundi la mashetani, lilikuwa hilo. Wanawake hao walikuwa uchi, wakiwa na kitu kilichochakaa chenye rangi ya kijivu, kama rangi ya ngozi ya ndovu. Nao walikuwa wamekishikilia mbele zao, bila sehemu yake ya juu hata kidogo. Nao walikuwa wakifanya upuuzi kama huu, ambao, hizi—hizi dansi ambazo hawa vijana hucheza hapa nje, kule kujisokota na mengineyo, na muziki kama huo ukiendelea. Na nilipoona Bi. Marekani amejitokeza, nusura nizamie.

<sup>202</sup> Sasa, hii ni BWANA ASEMA HIVI. Kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, niaminini sasa. Nisingesema hayo bure kamwe. Hamna fedha za kutosha ulimwenguni kote kunifanya nikasema hayo kama hayangalikuwa kweli.

<sup>203</sup> Basi alipopita huko, kilikuwa kitu kichafu kuliko vyote nilivyowahi kuona. Nikawaza, “Mungu, jinsi wahubiri na sisi ndugu tumejitahidi kukutafutia Wewe Bibi-arusi, na hivyo ndivyo vizuri tulivyoweza kufanya.” Alikuwa akijisokota-sokota, akishikilia *hiki* mbele zake, kama moja ya hizi sketi za dansi, akikishikilia mbele za sehemu zake, sehemu yake ya chini, *hivi*, huku akicheza dansi na kujisokota kama watoto hawa wafanyavyo huku nje kwenye. . . kwenye maonyesho haya ya kishenzi waliyo nayo, kujisokota. Huyu alikuwa Bi. Ukristo wa Marekani.

<sup>204</sup> Basi anisaidie, kwa msaada wa Mungu, hivyo ndivyo linavyoonekana machoni Pake. Ni—nilininii tu. . . nilianza. . . nusura nizamie. Niliwazia, “Kule kujaribu kwote, na kuhubiri, na kushawishi?” Kila mmoja wao amekata nywele, nao walikuwa wakijisokota na kupiga makelele, wakishikilia *hiki* mbele zao. Wakakaribia, pale nilipokuwa nimesimama pamoja na hiki Kiumbe cha kimbinguni. Singeweza kumwona Yeye. Ningemsikia akinizungumzia; alikuwa karibu sana nami. Bali walipogeuka upande *huu*, wanashika *hiki*. Huku wakijisokota tu na kucheka na kuendelea, kuendelea hivyo, wakishikilia *hiki* mbele yao.

<sup>205</sup> Sasa, mimi nikiwa nimesimama katika Uwepo Wake pale, nikiwa mtumishi Wake. “Na kwa yote yale niliyojaribu, hayo ndiyo bora sana niliyoweza kufanya?” Nikawaza, “Mungu, ilinifaidi nini? Ilifaidi nini? Kulia kwote, na kusih, na kushawishi, na zile ishara kuu na maajabu na miujiza ambayo Wewe ulionyesha. Na jinsi nilivyosimama pale, na kurudi nyumbani na kulia baada ya kuwahubiria hao na kadhalika, nayo ilinifaidi nini? Na kisha nikukabidhi Wewe kitu kama hicho, kama Bibi-arusi?”

<sup>206</sup> Nami niliposimama hapo, nikitazama, huyo bibi-arusi akapita. Nawe unaweza kuwazia upande wake wa nyuma, hamna kitu, akishikilia *hiki* mbele zake alipokuwa akijikokota huku akicheza dansi, namna hiyo, kwa mdundo huu wa

roki, akirusha-rusha viungo vyake namna hiyo. Na, yeye, loo, ilikuwa ya kishenzi, jinsi alivyokuwa akijiendesha, mwili wake ukitikiswa hivyo. Sasa mimi . . .

207 Unasema, “Ina maana gani, Ndugu Branham?” Sijui. Mimi ninawaambieni tu niliyoona.

208 Na huyo alipopita hivyo, nikamtazama. Loo, nikawa dhaifu kabisa. Nikageuka upande mwingine. Nikawaza, “Mungu, nimehukumiwa. Ha—hakuna haja ya mimi kujaribu chochote sasa. Hata afadhali niache.”

209 Bibi Carl Williams, kama unaketi hapa, na ile ndoto uliyoniambia, muda mfupi uliopita, uliyoota hivi majuzi usiku, ambayo imekuwa ikikusumbua, ndiyo hiyo. Usukani umeondolewa mikononi mwangu.

210 Basi, nikawaza tu, “Ni—ni heri hata nisahau hayo.” Nilikuwa nimekwisha.

211 Ndipo, mara moja, nikawasikia hao wakija tena. Basi upande *huu* akaja Bibi-arusi yule yule aliyekwenda upande *huu*. Hawa hapa wale wasichana wadogo wanakuja tena, na kila mmoja wao alikuwa amevalia vazi lao la taifa walikotoka, kama vile Uswisi, Ujerumani, na kwingineko, kila mmoja amevalia vazi kama hilo, wote wana nywele ndefu, vile vile hasa kama wale wa mwanzoni. Nao hawa hapa wanakuja, wakitembea. “Twendeni, askari Wakristo, kama waendao vitani.” Na wote walipopita kituo cha kukaguliwa kimbele ambapo tulikuwa tumesimama, mara, kila jicho likatazama upande ule. Ndipo wakageuka, nao wakaendelea, taratibu.

212 Na mara walipoanza kwenda moja kwa moja angani, huyu mwingine akapanda kwenye kilele cha kile kilima na kutelemka, *hivyo*.

213 Hawa nao wakaanza kupiga hatua hata angani. Na walipoendelea kupiga hatua, nikaona wasichana wadogo wachache huko nyuma, ilionekana kama kwamba huenda wakawa wasichana wa kigeni, kama Waswideni ama Waswisi, ama mahali fulani. Wakaanza kuangalia huku na huko, na ku- . . . Nikasema, “Msifanye hivyo! Msiache hatua hizo!” Na nilipopaza sauti namna hiyo, nikaja, kwenye lile ono, nimesimama pale huku mikono yangu imenyoshwa namna *hiyo*. Nikawaza, “Vema . . .”

214 Hiyo ndiyo sababu nikasema niliyosema, usiku wa leo. Nataka kuwaulizeni swali. Je, imechelewa kuliko tunavyodhania? Je, huenda ikawa tayari ameitwa na kuchaguliwa, akatiwa muhuri? Hapatakuwepo na mmoja zaidi, mwajua. Je, inawezekana? Loo, naam. Loo, naam.

215 Kumbukeni niliyosema, hivi majuzi kwenye kiamshakinywa. Kwenye chavua ya kuzalisha ya kiume na ya kike, kuna chembechembe hai milioni moja ambazo hutokea, mayai milioni

moja hutokea. Bali ni moja yao tu ambayo huishi, na, hata hivyo, zote zinafanana tu: moja katika milioni. Kila moja yao, ni yai lile lile na mbegu ile ile. Moja yao huishi. Zingine zote hufa.

<sup>216</sup> Hamna anayeweza kusema ni lipi kati ya mayai hayo lililo tayari, na, loo, chochote kulihusu. Inabidi Mungu kuamua hayo, kama itakuwa mvulana au msichana, mwenye nywele ya shaba ama nyeusi, ama chochote itakachokuwa. Mungu huamua hayo. Si ile ya kwanza kukutana, bali ya kwanza ambayo Mungu ameamua. Labda moja inakuja *hapa* juu, na moja. . . Kama umewahi kuchunguza, kwenye chupa ya kujaribia, kuona zikija pamoja. Nimezichunguza. Mungu hana budi kuamua hayo. Moja, kila moja, zinafanana kabisa, bali kwa kuchaguliwa. Kuzaliwa kwa kawaida ni kwa kuchaguliwa. Mungu huchagua mmoja kutoka kwa milioni.

<sup>217</sup> Israeli ilipotoka Misri, njiani mwao kuelekea nchi ya ahadi, walikuwa kadiri ya watu milioni mbili. Kila mmoja wao alikuwa chini ya mwana-kondoo yule yule wa sadaka, ama hawangaliishi. Kila mmoja wao alimsikiza Musa, nabii. Kila mmoja wao alibatizwa kwake, kwenye Bahari ya Shamu. Kila mmoja wao alicheza, wale wanawake pamoja na Miriamu, huku na huko kando ya (ambapo) ufuo wa bahari, Mungu alipomwagamiza yule adui. Kila mmoja wao alisimama pamoja na Musa, na kumsikia akiimba katika Roho. Wao, kila mmoja, walikula mana jangwani, iliyoshuka toka Mbinguni. Mana mpya, kila usiku, ambayo ni mfano wa Ujumbe, kila mmoja wao alikula hiyo. Lakini, kutoka kwa hao milioni mbili, wangapi walifaulu? Wawili. Mmoja kutoka kwa milioni moja.

<sup>218</sup> Kuna kama Wakristo milioni mia tano ulimwenguni usiku wa leo, tukihesabu Wakatoliki na wote. Milioni mia tano ya wanaojiita waaminio ulimwenguni. Kama Unyakuo ukitukia usiku wa leo, hiyo ingemaanisha. . . kama hesabu ingekuwa mmoja kutoka kwa milioni moja. Sisemi ndivyo. Bali ingelikuwa hivyo, watu mia tano, katika muda wa saa ishirini na nne zijazo, wangekosekana. Hata hungalisikia habari zake kamwe. Kutakuwa na kama hao watakaokosekana, haidhuru, ambao hata hawangejulikana waliko.

<sup>219</sup> Ndipo inawezekana, kutendeka kwetu, ewe rafiki, kama ilivyokuwa Yohana Mbatizaji alipokuja. Hata wanafunzi walisema, “Mbona Maandiko yakasema, mbona mi—mitume ama manabii wakasema, mbona inasema kwamba inampasa Eliya kuja kwanza na kutengeneza mambo yote?”

<sup>220</sup> Yeye akasema, “Nawaambieni ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wala hamkumtambua.”

<sup>221</sup> Mojawapo ya siku hizi tunaweza kuachwa tumeketi hapa, “Vipi kuhusu Unyakuo kabla ile dhiki kuu kuja?”

“Umekwisha kuja nanyi msitambue.”



222 Mwili wote, umetiwa muhuri, unapiga tu hatua. Sisemi hivyo ndivyo ilivyo. Natumai sivyo ilivyo. Lakini, ewe rafiki, inapoachilia. . .

223 Kama tunajisikia moyoni mwetu, usiku wa leo, ya kwamba inatupasa kulainisha maisha yetu, na mambo ambayo tumefanya, hebu niwashauri, kama ndugu mhudumu. Nitasema haya kwa mara yangu ya kwanza, mimbarani. Nimeenda kirefu zaidi usiku wa leo, juu ya *Huu*, kuliko nilivyowahi kufanya juu ya chochote kingine, wakati wowote, kwa vyovyote, hadharani, kwa sababu nimekuwa huru sana kwenye mikutano hii. Kama unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, sikiliza yale niliyokwambia. Kama una hata mlío mdogo wa hisia moyoni mwako, wewe mwende Mungu sasa hivi. Fanya hivyo.

224 Simama kidogo tu, enyi wanaume. Chunguza ninii zako—kanuni zako za imani unazotumikia. Angalieni makanisani mwenu. Je, yameambatana kabisa na Neno la Mungu? Je, umetimiza masharti yote? Unasema, “Mimi ni mtu mzuri.” Vivyo hivyo Nikodemo, na vivyo hivyo wengine wote. Wa—walikuwa wazuri. Unaona? Hilo halihusiani Nalo hata kidogo.

225 Nanyi, wanawake, nawatakeni mtazame kwenye kioo, na muone yale Mungu anahitaji mwanamke kufanya. Na utazame kwenye kioo cha Mungu, si katika kioo cha kanisa lako sasa, katika kioo cha Mungu; na uone kama ungalihitimu, katika maisha yako, kuwa Bibi-arusi wa kiroho wa Yesu Kristo.

226 Wahudumu, wazeni vivyo hivyo. Je, wewe hupiga kona *hapa*, kusudi usimuudhi mtu fulani mle? Je, ungefanya *hivi* kama haikuwa. . . nao watakufukuza kanisani? Kama unajisikia hivyo, ndugu yangu mpendwa, hebu nikuonye, katika Jina la Yesu Kristo, yakimbie hayo sasa hivi.

227 Nawe, mama, iwapo huwezi kutimiza masharti ya Mkristo, si kama Mkristo wa kawaida, bali moyoni mwako, na maisha yako yanalingana kabisa na cheti cha Mungu cha arusi, hapa, kinasema yanapaswa kuwa. . .

228 Nawe, mshiriki wa kanisa, iwapo kanisa lako haliko hivyo, halitimizi masharti ya Mungu ya Neno Lake, toka kwake ukaingie ndani ya Kristo.

229 Hilo ni onyo zito. Hatujui ni wakati gani, nanyi hamjui ni wakati gani, ambao mji huu siku moja utakuwa umezama humu chini ya bahari hii.

230 “Loo, Kapernaumu,” Yesu akasema, “ewe uliyetukuzwa mpaka mbinguni, utashushwa mpaka kuzimu. Kwa kuwa, kama ile miujiza ingalifanyika katika Sodoma na Gomora, ingalikuwako hata leo.” Na Sodoma, Gomora imezama chini ya Bahari ya Chumvi. Na Kapernaumu uko chini ya bahari.

231 Ewe mji, unayejidai kuwa mji wa Malaika, ambao umejikuza mpaka mbinguni, na kupeleka mambo yote machafu, ya mitindo

na mengineyo, mpaka hata nchi za ng'ambo huja hapa kuokota uchafu wetu na kuupeleka mbali, kwenye makanisa yako mazuri na minara, na mengineyo, jinsi ufanyavyo. Kumbuka, siku moja utazama chini ya bahari, masega yako makuu yako chini yako sasa hivi. Ghadhabu ya Mungu inakokomoa papa hapa chini yako. Ni muda gani atazuia ufuko huu unaoning'inia kule? Wakati, ile bahari kule ng'ambo, yenye kina cha maili moja, itakopotiririka mle, kote kote mpaka kwenye Bahari ya Salton. Itakuwa mbaya zaidi kuliko siku ya mwisho wa Pompeii. Tubu, Los Angeles.

<sup>232</sup> Tubuni, ninyi wengine, mkamrudie Mungu. Ile saa ya ghadhabu Yake iko juu ya nchi. Kimbieni wakati kungali na wakati wa kukimbia, na mwingine ndani ya Kristo.

Na tuombe.

<sup>233</sup> Mungu mpendwa, huku, katika roho yangu, ninatetemeka, moyo wangu unadondoka machozi ya maonyo. Jalia, Ee Mungu, ya kwamba wanaume na wanawake hawatachukulia yale nimesema kuwa ni mchezo, na watu wa kanisa wasiyadhani kwamba ni maonevu au kuwapinga. Jalia waone, Bwana, ni katika upendo.

<sup>234</sup> Wewe unanishuhudia, Mungu Mwenyezi, ya kwamba nimeenda huku na huko katika pwani hii, mwaka baada ya mwaka, nikitangaza Neno Lako. Nishuhudie, Ee Mungu, kama ingalitendeka usiku wa leo, nimewaambia yaliyo Kweli. Wewe unajua ono hili la Bibi-arusi ni Kweli. Nimechukua Jina Lako kwake, Bwana, na kusema ilikuwa BWANA ASEMA HIVI. Nami ninajisikia ya kwamba ninajua, Bwana, ninayofanya.

<sup>235</sup> Kwa hivyo nakuomba Wewe, Bwana, katika Jina la Yesu, hebu na watu wajitikise, usiku wa leo, na kuikimbia ghadhabu inayokuja, kwa maana Ikabodi imeandikwa kwenye milango na juu ya mataifa. Alama nyeusi ya kukataliwa imetiwa kwake. Roho wa Mungu amehuzunishwa akaondoka kwake, nao wamepimwa katika mizani wakaonekana kuwa wamepungukiwa. Ile karamu ya mfalme Nebukadreza imejirudia tena, pamoja na karamu za ulevi na wanawake walio nusu uchi, wakijiita Wakristo.

<sup>236</sup> Ee Mungu wa Mbinguni, hurumia ulimwengu wenye dhambi na watu wenye dhambi, Bwana, kama tulivyo usiku wa leo. Mungu, ninajaribu kusimama pengoni na kuomba rehema ya Kiungu, kwamba utalizungumzia kundi hili usiku wa leo na kumhamasisha Bibi-arusi Wako, Bwana, akapige hatua taratibu si kwa ishara za kanuni zozote za imani, bali kwa sauti ya Injili ya Bwana Yesu Kristo. Tujalie, Ee Mungu. Na ijulikane, usiku wa leo, ya kwamba Wewe ni Mungu, na Neno Lako ni Kweli. Huku, kwa uchaji, mbele ya macho ya watu hawa, tunawahamasisha Neno Lako.

237 Katika Jina la Yesu Kristo, nawaombea, Bwana. Wao wamekuona Wewe, bila shaka lolote, ukitembea kwenye umati wa watu na kuwaambia yaliyo moyoni mwao. Nawe unajua, Bwana, yale, yanayoendelea, hivi sasa. Unajua hiyo ni Kweli, Ee Mungu. Nami nakuomba, katika Jina la Yesu, jalia Roho Mtakatifu atuombea tena, Bwana, na akavute kutoka kwa wasikilizaji hawa, Bwana, wale walioandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Tujalie, Ee Mungu. Naomba kwa moyo wangu wote.

238 Watu hawa, kwa kawaida, Bwana, wangenipa mimi senti ya mwisho waliyokuwa nayo, kusudi wausaidie huu Ujumbe. Wangalifanya chochote wangaliweza. Bali, Ee Mungu, ifikiapo kuambatana Nao, na kuingia ndani Yake, naomba, Mungu, ya kwamba huu utakuwa usiku ambao utawatuza na kumwaga Roho Wako Mtakatifu juu ya mkutano huu. Na kusiwe na mchezo ama kurukaruka huku na huku, bali maombolezo na kilio, na kutubu, kushikilia zile pembe za madhabahu, tunapooona hukumu zikimiminika chini yetu, usiku wa leo. Tujalie, Mungu. Naomba kwa unyenyekevu nijuavyo, katika Jina la Yesu Kristo.

239 Ndugu yangu, dada, si—sijui niseme nini zaidi, iwapo nimepata neema machoni penu, kwa uweza wa Mungu, kama mnaniamini mimi kuwa nabii Wake. Hii ndiyo mara yangu ya kwanza kusema hilo hadharani. Bali nasikia onyo geni la namna fulani. Mimi sizoelei haya. Mnajua hivyo. Mimi sitendi hivi. Nalisitasita kutoa Ujumbe huo na kusema mambo hayo. Naliyakwepa na kadhalika, nisije nikafanya hivyo. Bali yashasemwa, nayo yatasimama kwenye ile Siku ya Hukumu, kama ushuhuda ya kwamba nimesema Kweli. Hiyoni ni BWANA MUNGU ASEMA HIVI! . . . ? . . .


240 Enyi, Pentekoste, kimbieni kwa ajili ya maisha yenu. Kimbilieni zile pembe za madhabahu mkalie, kabla haijachelewa sana, kwa kuwa saa yaja ambapo mnaweza kulia na haitawafaa kitu. Kwa kuwa Esau alitafuta apate mahali, pa haki yake ya mzaliwa wa kwanza, asipate. Nakukabidhi, ewe, California. Enyi, mkutano wa Wafanyi Biashara wa Full Gospel, ambao nawapenda, ambao nimewaacha na kuwakumbatia, kwa moyo wangu wote, nawakabidhi kwa Yesu Kristo, usiku wa leo. Mkimbilieni Yeye! Msimwache ibilisi awapoeshe kutoka kwa Hili. Kaeni Nalo daima hata mtakapokuwa, mmejazwa na Roho Mtakatifu, sana, kila mmoja wenu, hata itakufanya uje kwa hili Neno, litakalowafanya enyi wanawake mjitengeneze, litakalowafanya enyi wanaume mjitengeneze. Kama ukisema ya kwamba una Roho Mtakatifu, na huwezi kuambatana na Neno, ni roho mwingine aliye ndani yako. Roho wa Mungu yuko kwenye Neno Lake, Umasihi, Neno lililopakwa mafuta. Bibi-arusi hana budi kuwa Masihi mdogo, Neno lililopakwa mafuta.

<sup>241</sup> Hebu na tusimameni kwa miguu yetu, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Kama hutaisikia sauti yangu tena... Lakini, Mungu akipenda, ninaondoka kwenda Afrika, katika muda wa saa chache. Huenda nisirudi kamwe. Sijui. Bali nawaambieni, kwa moyo wangu wote, nimewaambia Kweli. Sijaacha kuwatangazieni kila kitu ambacho Mungu ameniambia niseme. Nami nimesema Hayo katika Jina la Bwana.

<sup>242</sup> Ni wakati mzito mno. Sijui namna ya kuieleza. Nimejaribu kuondoka mimbarani mara tatu ama nne, na sikuweza kufanya hivyo. Hii ni saa ya uchaji sana. Usiisahau kamwe. Huu ni wakati ambao, labda, Mungu huenda anaita kwa mara Yake ya mwisho. Sijui. Yeye atafanya wito Wake wa mwisho, siku moja. Lini? Sijui. Bali nawaambieni, kulingana na ono hilo, inaonekana kama huyo Bibi-arusi karibu ameshakamilika.

<sup>243</sup> Yaangalie yale makanisa ya kawaida yakiingia. Wakati mwanamwali aliyelala alipokuja kutafuta Mafuta, hakuyapata. Bibi-arusi akaingia. Unyakuo ukapaa juu. "Walipoondoka kwenda wakanunue Mafuta, Bwana-arusi akaja."

<sup>244</sup> Je, mmelala? Amkeni, upesi, mjirudie. Na hebu tuombe, kila mmoja, kama kwamba tunakufa dakika hii, katika Jina la Bwana. Hebu, kila mmoja, omba kwa njia yako mwenyewe.

<sup>245</sup> Mungu Mwenyezi, uturehemu. Bwana, nirehemu mimi. Turehemu sisi sote. Inatufaidi nini, haijalishi tufanyacho, kama tukikosea katika mambo haya? Nasimama na kukuomba rehema, Ee Mungu, kabla mji huu mkuu haujazama chini ya bahari na hukumu za Mungu kuenea kwenye pwani hii. Naomba, Mungu, ya kwamba Wewe utamwita Bibi-arusi Wako. Nawakabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Amina. 

*KUCHAGUA BIBI-ARUSI* SWA65-0429E  
(The Choosing Of A Bride)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 29 Aprili, 1965, kwa ajili ya mkutano wa ushirika wa kimataifa wa Wafanya Biashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Biltmore, huko Los Angeles, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)